

# Wengine

## MASOMO YA BIBLIA YA WANAWAKE – MAKAO MAKUU YA KIMATAIFA



# Wengine

MASOMO YA BIBLIA YA WANAWAKE –
MAKAO MAKUU YA KIMATAIFA



# UTANGULIZI

**WAPENDWA MARAFIKI KATIKA KRISTO,**

Nafurahi kuweza kuwasilisha kwenu mkusanyiko wa masomo ya Biblia ya mwaka 2023 kutoka Huduma za Kimataifa za Wanawake, *Wengine.* Ni imani yangu thabiti kwamba Mungu anatuita tutembee na wengine; kwa kujiamini, kwa ujasiri, kwa kuaminiana na kwa uthabiti. Mioyo yetu itabakia imeunganishwa na Mungu, lakini mikono yetu lazima iwafikie akina mama, wasichana, wanaume na wavulana, duniani kote. Kuwapenda wengine ni mwito wa Mungu tuingie kazini kwa ajili ya maisha yetu!

Lakini, zaidi ya kuwazungumzia wengine, tunatakiwa kwa kweli tutoke nje na tuungane nao katika roho ya jamii ya makusudi, kuwasikiliza watu wanapopaza sauti kuhusu mahangaiko na furaha zao. Kwako, hii inaweza kuonekana kama kuzungumza na kuelimisha kuhusu ukosefu wa haki, au kuwasaidia wengine katika njia za matendo na maombi kupita katika nyakati za uharibifu. Labda, katika maisha yako, kuishi katika jamii pamoja na wengine ni kama mfululizo wa nafasi za kufanya mazoezi ya kukumbatia utamaduni na mitazamo mipya.

Hadithi inaelezwa ya mwanzilishi wa Jeshi la Wokovu, Jenerali William Booth, alipokuwa mzee. Inaelezea umuhimu wa mada hii kwenye huduma yetu. Mwanzilishi alitegemewa kuhubiri katika mkutano mkubwa, lakini hali yake kiafya ilifanya asiweze kuhudhuria na badala yake akatuma ujumbe wa simu kwa maandishi. Maelfu walikusanyika kwenye tukio, wakiwa na hamu ya kumsikiliza mhubiri maarufu akihubiri. Usiku huo, mjumbe aliifungua simu ya maandishi iliyokuwa imefungwa na umati wa watu ulikuwa kimya kwa matarajio. Mlikuwa na neno moja tu lililoandikwa humo, 'WENGINE!'

Mwito wa Jenerali Brian Peddle unahimiza waumini wa Jeshi la Wokovu 'wahusike', wawe 'tayari kwa vita' na 'wawajibike'. Akitafakari kuhusu mwito wa upendo unaojumuisha, aliandika, 'Tunatakiwa kuwa juu zaidi ya lawama katika kuwatendea watu wote kwa heshima na huruma, tukikumbuka huduma yetu ya kukutana na mahitaji ya wanadamu katika jina la Kristo bila ya ubaguzi.' Ni katika kujibu changamoto hiyo mkusanyiko huu wa masomo ya Biblia, Wengine, umetengenezwa. Masomo haya yanazingatia namna gani tunahitajika kuwa tayari, tunakumbatia na kuwezesha kwenda nje na kuwapenda wengine, kuwaonyesha wanapendwa na Mungu, na kuwakaribisha ndani ya Jeshi la Wokovu. Tukisaidiwa na maelekezo yaliyotolewa kwa ajili yetu katika 1 Wakorintho 13, mkusanyiko huu inaonyesha upendo ambao 'haukosi kuwa na adabu kwa wengine' (1 Wakorintho 13:5).

Kutokana na mwito huu wafuasi wa Kristo bila shaka wanabakia na kuwapenda wengine. Tunapowapenda watu wengine vizuri, utambulisho wetu wa kweli wa Kristo utadhihirika. Yesu anatuita tujazwe upendo kwa ajili yake na, kutokana na upendo huo, tutakuwa tukimsogelea karibu zaidi: 'Amri mpya nawapa: mpendane... hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi' (Yohana 13:34-35).

Maombi yangu juu ya mkusanyiko huu wa masomo ni kwamba kila mmoja atakayehusika na maneno haya ataona uwepo wa Mungu ukihudumia mioyo yenu. Naomba kwamba, kutoka kwenye kufurika kwa Roho

Mtakatifu, wengine watakuwa na watabakia kuwa zingatio la huduma yetu. Naomba vile vile kwamba mkusanyiko wenyewe utakuwa mahali pa mjumuisho wa mioyo inayo mheshimu Mungu na kuwa heshimu wengine wajumuike. Masomo haya yameandaliwa na waandishi wanawake, lakini hayakusudiwi yatumike na makundi ya wanawake peke yake. Naomba kwamba masomo haya yatumike katika vikundi vinavyohudumia rika zote, tamaduni, mataifa, lugha na jinsia, ili Kanisa liutukuze utajiri na uzuri wa Mungu muumba!

Tunataka kushuhudia ukweli unaowezesha na ujasiri wa Roho Mtakatifu. Tunajua kwamba yeye anaweza kutuwezesha sisi kuwa sauti yake, mikono yake, na miguu yake katika ulimwengu unaotafuta tumaini, ukweli, mabadiliko na amani!

Mungu akubariki unaposoma.

**‘TUNAPOWAPENDA VIZURI WATU WENGINE, UTAMBULISHO WETU WA KWELI WA KRISTO UTADHIHIRISHWA.’**

**Kamishena Rosalie Peddle**
**Rais wa Huduma za Wanawake**

# KUTEMBEA KUPITA SAMARIA

YOHANA 4:3-9

MEJA AMY REARDON

Unaposoma vifungu vya somo hili la Biblia, unaweza kushangazwa kuona kwamba ni vifungu vya 3-9 tu vya sura hii maarufu ndivyo vinakumbukwa. Sehemu kubwa ya kukutana kwa mwanamke Msamaria na Yesu bado haijajifunua. Hata hivyo, jambo muhimu tayari limekwisha kutendeka. Sura inaonyesha jinsi ambavyo Yesu alimthamini hata mtu wa chini sana katika mfumo wa jamii wa kale wa Wapalestina – mwanamke aliye fedheheshwa. Lakini mwanzo wa sura hiyo unaonyesha vile vile kwamba Yesu hakuwa na ubaguzi wa rangi wala utamaduni.

Mwaka 722 Kabla ya Kristo, taifa kuu la Ashuru liliteka Ufalme wa Kaskazini la Israeli. Mfalme wa Ashuru alipeleka raia wake wengi huko. Waisraeli na Waashuru katika eneo hilo wakaanza kuoana. Wakati wa Yesu eneo hilo lilijulikana kama Samaria. Wayahudi wa karne ya kwanza waliwadharau Wasamaria kwa sababu mababu zao walidhoofisha damu ya Waebrania na imani kutokana na kuoana na usawazishaji wa dini. Walikuwa watu mchanganyiko, uzao wa 'wasio safi'.

## 'SISI TUNATAKIWA KUMUIGA YESU, KWA MIOYO ILIYO WAZI KWA AJILI YA TAIFA NA TAMADUNI ZOTE HATA IWEZE KUWAPA WATU MSHANGAO.'

Yohana 4:3-4 ina twambia kwamba Yesu alikuwa anatoka Uyahudi akielekea Galilaya,na kwamba 'alilazimika kupitia Samaria'. Hii inafanya mtu atake kujua, kwa sababu haikuwepo sababu ya Yesu kulazimika kwenda kupitia Samaria. Wayahudi walisafiri kutoka Uyahudi kwenda Galilaya wakati wote, lakini hawakupitia Samaria. Waliizunguka, wakiongeza umbali na matatizo kwa safari zao.


Katika kitabu chake 'Shahidi wa kuaminika' (*A Credible Witness)*, Brenda Salter McNeil anasema, 'naamini kwamba Yesu "alilazimika" kwenda kupitia Samaria kwa sababu alilazimishwa na moyo wa Baba' (ukurasa wa 42). Wakati kutembea kupita Samaria lilikuwa jambo wasilofikiria Wayahudi wengi, lakini ilikuwa dhahiri ni tendo la kusudi la Yesu. Alijipanga kuonyesha kwamba watu wote walikuwa na thamani sawa.

Kuna matendo matatu ya Yesu katika vifungu hivi ambayo tunaweza kuiga.

### 1. YESU ALITHUBUTU KUINGIA ENEO LA 'KIGENI'.

Milango ya makanisa na nyumba zetu lazima ifunguliwe kwa watu wote, hasa katika wakati huu ambapo tamaduni nyingi na mataifa wanachangia eneo moja kijografia. Zaidi ya hilo, tunatakiwa tutoke katika maeneo yetu twende kwa majirani tukiwa na mioyo iliyo wazi, tukiwa tayari kujifunza na kupenda. Sababu moja ya hili ni kuwashirikisha wengine imani yetu kwa umbali na kwa upana kama tuwezavyo. Hatujaitwa tuwape kisogo wale ambao wako tofauti na sisi. Tumeitwa 'twende ulimwenguni mwote, tukaihubiri Injili kwa kila kiumbe' (Marko 16:15).

Tuna kwenda katika maeneo mengine ili tuwaelewe vizuri kaka na dada zetu katika Kristo. Nakumbuka wakati waumini wa kikao cha huko Chile walipohudhuria karibu na Washington, D.C., Marekani, walituchukua baadhi yetu Wamarekani ya Kaskazini kwenye hoteli iliyopika chakula cha watu wa asili. Ni watu wawili tu kati ya watu 20 waliokuwa wanazungumza Kihispania na Kiingereza. Hata hivyo tuliweza kuuona upendo na furaha ya Kristo kati yetu.



## JADILI:

* Unaweza kufanya jitihada zipi kuchunguza utamaduni mwingine?
* Je, ndani yako mna hisia mbaya juu ya watu wa rangi au utamaduni mwingine? Uko tayari kutubu na kumwomba Bwana aubadilishe moyo wako?

### 2. YESU ALICHAGUA MAHALI AMBAPO TAMADUNI ZAO ZOTE ZILIUNGANA.

Kukutana huku katika Yohana 4 kulifanyika kwenye kisima cha Yakobo. Wasamaria na Wayahudi wa asili walichangia vyanzo na makundi yote wali waheshimu baba zao waliotangulia, Yakobo. Ni busara kukumbuka kwamba kama binadamu tunayo mengi ya kufanana. Sote tunapenda sana familia zetu, tunafurahia kicheko kizuri na tunataka maisha yetu yawe na maana. Kufanana kwetu kunashuhudia kwamba hayupo aliye bora zaidi ya mwingine, na tunaweza kupata mahali pa kuanzia mazungumzo.

Wakati mume wangu na mimi tulikuwa maafisa wa kikao cha Seattle, Washington, kikao chetu kilikuwa na askari wachache kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Huko nyumbani kwao chombo cha kutolea sadaka hakikuwa kinapitishwa kama sisi tulivyozoea; watu hucheza wakija kutoa sadaka zao kwa Bwana. Tulijaribu hili huko Seattle na askari wetu walipenda kupiga makofi na kuimba na kucheza sana hata tukaamua kulifanya hili mara moja kwa mwezi. Zaka ilikuwa tayari ni nidhamu ya pamoja, lakini tulifungua mioyo yetu na tukapata njia mpya ya kulifanya hili.

### 3. YESU ALIONYESHA USHIRIKA WA KWELI


Moja ya mambo ya kustaajabisha sana yaliyofanywa na Yesu katika vifungu vyetu vya Yohana 4 ilikuwa ni kuomba maji ya kunywa. Tony Evans anaandika: ‘Kuweka midomo yake kwenye kikombe cha Msamaria ilikuwa ni tendo la ushirika wa karibu na kukubalika kwa dhati’ (‘umoja umekumbatiwa’ *Oneness Embraced*, ukurasa wa 61).

Wakati mume wangu na mimi tuliwachukua watoto wawili ambao hawakuwa wadogo na kuwafanya wa kwetu, mara ya kwanza nilitulia kwa muda nilipochangia kikombe na wao. Mara nyingi nilichangia kikombe na watoto niliowazaa mwenyewe, lakini ulikuwepo wakati tulipokuwa na watoto wetu tuliowachukua kungine ambao kiwango hicho cha ukaribu kilitakiwa kujengwa. Naweza kufikiria tu mshangao alioupata mwanamke Msamaria wakati Myahudi – aliyetakiwa kufikiria kwamba yeye mwanamke Msamaria alikuwa anasikitisha – aliomba anywee kikombe chake.

Tunaweza tusichangie vikombe, lakini ni mfano wa namna gani ambao Yesu alituonyesha! Sisi tunatakiwa kumuiga Yesu, tukiwa na mioyo iliyofunguka kwa watu wa mataifa yote na tamaduni zote hata iwezekane kuwashangaza watu. Hebu na tuwe tayari kutembea kupitia Samaria.

Ewe Yesu, tufundishe kuwaelewa na kuwaheshimu watu wote uliowaumba. Unatupenda sote kwa usawa. Tusaidie na sisi tufanye hivyo.


**MEJA AMY REARDON**
MAREKANI YA MAGHARIBI
Meja Amy Reardon ni Msaidizi wa Mkuu wa chuo cha mafunzo California.
Ni mama wa watoto watano na hivi karibuni alikuwa bibi.

# KUMWAMINI MUNGU KATIKA MAZINGIRA YOTE

YEREMIA 29:11

KAPTENI ASTRID CHRISTENSEN

'"Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani, wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho"' (Yeremia 29:11).

Yeremia ni mmoja wa manabii wa kuu katika Biblia, ingawa ni wa kusita sita. Alikuwa vile vile anakabiliwa na msongo wa mawazo.

Licha ya kutokuwa radhi yeye, Yeremia ni mwaminifu kwa mwito wake. Ameitwa na Mungu kuwapa unabii watu. Amepewa jukumu la kuwambia watu wanaishi katika dhambi na ni lazima watubu, ama sivyo watapelekwa uhamishoni. Watu hawakutubu, na kwa hiyo walifukuzwa kutoka katika nchi yao, vile vile kama Yeremia alivyotabiri.

Watu walichukuliwa mpaka Babeli walikoishi uhamishoni. Hawakutaka kuishi Babeli. Wakaikosa sana Yerusalemu – Sayuni yao inayopendwa.

Mungu anaongea na Yeremia na kumwambia awaambie watu kwamba wanatakiwa kujenga nyumba na waishi ndani yake, wapande bustani na wale matunda yake. Wataoa na kuwa na watoto wa kike na wa kiume, na watoto wao wa kiume na wa kike wataoa na kuolewa ili wawe na watoto. Wataongezeka kwa idadi – hawatapungua. Watatafuta furaha na maendeleo katika mji wanamokaa, na mji unapoendelea, wao pia wataendelea.

Kupitia kwa Yeremia, watu wanaambiwa kwamba miaka 70 itapita kabla ya ahadi ya kurudi kwenye nchi yao wenyewe haijatimia.

## 'LAZIMA TUZINGATIE KUFANYA KILE KILICHO SAHIHI MBELE ZA MUNGU. KWA KUJENGA KILA ANACHOKIWEKA KATIKA MIOYO NA AKILI ZETU.'

Watu wanakumbushwa maneno '"Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani, wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho."'


Ni kifungu kinachofahamika sana, lakini hutumika visivyo mara nyingi.

Tunapo kisoma kifungu hiki, tuna mazoea ya kukitafsiri kama kinazungumzia kuhusu furaha ya papo. Kwamba Mungu anaingia kwenye hali yetu mara moja, na kwamba hitaji letu la furaha litashughulikiwa mara moja hapa na sasa. Lakini haya siyo yanayozungumzwa na hiki kifungu.

Kama tukikitazama kifungu kwa karibu, tutaona kwamba kilisemwa kwa watu ambao wako chini ya shinikizo kubwa. Wamo katika nchi ambayo hawataki kuwamo ndani yake. Wapo chini ya utawala ambao hawataki kuwa chini yake. Wamefukuzwa wakaenda katika nchi nyingine. Hapa Mungu anawaambia watakaa hapo kwa miaka 70 kabla ahadi haijatimia.

Kutegemea ni wapi tunaishi duniani, maisha yetu yanaweza kuathiriwa na kutokuwa na utulivu, msongo wa mawazo, talaka, wasiwasi, umaskini, mateso, magonjwa, vita au kukata tamaa. Vile vile kama Wayahudi uhamishoni Babeli, watu wa leo wanajua nini maana ya kuwa chini ya shinikizo, na kuwa katika mazingira ambamo hawataki kuwamo.

Zaidi sana, haijalishi tuko wapi duniani, tunaweza kujisikia kwamba tuko uhamishoni, na tunaweza kuhusisha na jinsi Wayahudi walivyojisikia.



## JADILI:

* Tunaweza kujifunza nini kutoka kwa Yeremia 29 kuhusu kuishi mahali tulipo?
* Kuna maeneo katika maisha yako yanayokufanya usiwe salama na kusababisha usiishi maisha yako kikamilifu?
* Unahitaji kukumbatia ahadi ya Mungu ya tumaini na ya siku zijazo? Unaweza kuweka nini katika mikono ya Yesu na umwamini yeye kwa hayo?

Katika Wafilipi 3:20 tunasoma: 'Kwa maana, sisi wenyeji wetu uko mbinguni, kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo.'

Tumeumbwa kuishi pamoja na Mungu, lakini tunapokuwa tungali hapa duniani, tutajisikia kutengwa na Mungu kiasi fulani, na hapo ndipo hisia za kuwa uhamishoni huja.

Katika maisha yetu, tunaweza kujikuta mahali au katika mazingira ambayo hatutaki tuwemo. Tunaweza kujikuta tumo katika shinikizo katika mazingira mbalimbali, na wakati mwingine inaweza kuonekana kuwa kama hakuna maendeleo au tumaini kwetu sisi.

Huenda uko katika shinikizo leo, katika huduma yako, katika ndoa yako, katika maisha ya familia yako, kazini kwako, shuleni, au kuna jambo katika jamii yako linaloweka shinikizo juu yako.

Yeremia alizungumza kwa watu waliokuwa uhamishoni, nao waliambiwa waishi maisha yao licha ya kuwa mahali hawapataki. Walitiwa moyo wapanue mji, ambao wangetamani wauhame. Wanatakiwa kuishi maisha yao, na wanatakiwa kutengeneza maisha mapya mengine. Wanatakiwa kuweka mizizi, wakifahamu vema kwamba siku moja ahadi ya kurudi nyumbani kwao itatimia.

Lazima tuzingatie kufanya kile kilicho sahihi mbele za Mungu. Kwa kujenga kila analoliweka katika mioyo na akili zetu. Kwa njia ile ile, kifungu kinazungumza nasi leo. Haijalishi tuko wapi, haijalishi tunafananaje – haijalishi tuna hali gani – maneno yale yale yanazungumza nasi leo.

Uwepo wetu katika jamii ambayo tumewekwa ndani yake, na kati ya watu tuliowekwa pamoja nao. Tunatakiwa kufanya vema kwa furaha na kuamini kwamba tutabarikiwa kwa sababu ya hilo. Huku tukiweka macho yetu nyumbani kwetu halisi na uraia wetu wa kweli; uraia wetu na nyumbani kwetu na Mungu.

Ahadi waliyopewa Wayahudi: "Maana ninayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani, wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho", yanatumika leo vile vile.

Mungu ni Baba yetu, anayeheshimu ahadi zake. Hii ni ahadi nzuri kwetu, kwamba bila kujali ni mazingra gani tuliyomo, Mungu ana mipango mikubwa na maisha yetu. Ni maisha yenye tumaini na maendeleo. Tunapotulia katika ahadi hii tunaweza kutenda kikamilifu na kuwafikia wengine kwa upendo na tumaini.

Ni siku zijazo ambazo Mungu amezipanga kwa ajili yetu toka mwanzo.

Nakushukuru, Mungu Baba yangu, kwamba una mipango ya tumaini na siku zijazo kwa ajili yangu. Haijalishi ninavyojisikia, na haijalishi mazingira yangu, najua unanitia moyo nikuamini na kuamini ahadi ulizonipa mimi. Amina.

**KAPTENI ASTRID CHRISTENSEN**
DENMARK NA GREENLAND
Natumika Tønder, Denmark, nafanya kazi na familia zilizo katika mazingira hatarishi. Tumeoana na Strange, ambaye na yeye ni Kapteni. Tuna watoto watano, wenye umri ufuatao 19, 17, 15 na mapacha wa miaka tisa. Tulipata mwito wa kumtumikia Bwana ndani ya Jeshi la Wokovu miaka 11 iliyopita.



# TOFAUTI YA VIZAZI

WAKOLOSAI 1:16-17

KAPTENI DOROTHY CHRISTOPHER MACWAN

Mungu siku zote ametufundisha kuwapenda wengine na kuheshimu na kuwajumuisha watu wote. Tukisahau au tukidharau hili, tuna matokeo mabaya.

Moja ya matokeo ni pengo la vizazi. Pengo la vizazi ni ile tofauti ya mienendo kati ya watu wa vizazi mbalimbali, kinacho sababisha pawepo kutoelewa. Inaweza kuonekana katika sehemu ya kazi, ndani ya familia, katika jamii zetu na katika huduma yetu. Inaweza kusababisha sisi tupuuze thamani ya mtu kwa sababu ya umri wake.


Hata hivyo, tofauti ya vizazi ni mpango wa Mungu. Kote katika Biblia tunaona picha maridadi ya tofauti za vizazi zinazothibitisha jinsi ambavyo Mungu huwaita watu wa umri mbalimbali wakamilishe kazi yake. Mungu alimlinda mtoto mchanga Musa ambaye baadaye alikuja kuwa kiongozi wa Waisraeli. Mungu alimtumia Samweli, kijana mdogo, kuwa mjumbe wa familia ya Eli. Kama mzee, Mungu alimtumia Musa kuwakomboa Waisraeli kutoka utumwani.

Kitabu cha Kutoka kinatoa mfano mkubwa wa tofauti ya vizazi. Mungu aliwakomboa na akawaongoza watu wa Mungu waliochaguliwa kwenda nchi ya ahadi huku akiwakumbatia vijana kama Yoshua na Kalebu, aliowaona kuwa wenye thamani katika kukamilisha kazi ambayo Mungu amempa. Musa vile vile alikuwa anawaandaa kwa uongozi, na Yoshua alikuja kuwa kiongozi mzuri baada ya kifo cha Musa.

Watu wa vizazi vyote wana umuhimu sawa mbele za Mungu. Kujumuishwa kwa vizazi mbalimbali huwafanya watu wajisikie wanaheshimiwa, wana thamani na wana karibishwa. Huinua kujiamini na kuwasaidia watu watambue thamani yao wenyewe.

1 Wakorintho 12:12-14 inasema: 'Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi ni mwili mmoja, vivyo hivyo na Kristo. Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi au kwamba tu Wayunani, ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru, nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja. Kwa maana mwili si kiungo kimoja, bali ni vingi.'

**'KOTE KATIKA BIBLIA TUNAONA PICHA MARIDADI YA TOFAUTI ZA VIZAZI ZINAZOTHIBITISHA JINSI AMBAVYO MUNGU HUWAITA WATU WA UMRI MBALIMBALI WAKAMILISHE KAZI YAKE.'**



**JADILI:**

* Unawajumuisha na kuwaheshimu watu wa umri mbalimbali namna gani katika familia, jamii na kanisa lako?
* Picha ya tofauti za vizazi katika kanisa lako na familia yako ni ipi?

Mwili wa binadamu una viungo vingi vinavyofanya kazi kwa pamoja kuweka mwili uwe na afya na unaofanya kazi. Kwa njia ile ile, sisi waumini kanisani – wana familia ya Mungu, wa umri na mataifa mbalimbali, na karama mbalimbali – tunatakiwa kufanya kazi kwa kushirikiana mmoja na mwingine, kwa kuheshimiana, kupendana, kutiana moyo na kuonyesha tunajaliana sisi kwa sisi, kama sehemu ya mwili mmoja wa Kristo. Kutegemeana kwetu sio udhaifu; na kunatufundisha tuingize, upendo na heshima mmoja kwa mwingine na kwamba tunahitajiana ili tutimize kusudi tulilopewa na Mungu. Kuna aina mbalimbali za karama, lakini Rohoni ni yule yule anayezigawa.

Kuna aina mbalimbali za huduma, lakini Bwana ni yule yule. Kuna aina nyingi za kufanya kazi, lakini zote na katika kila moja ni Mungu yule yule aliye kazini (1 Wakorintho 12:4-6). Hebu hii itukumbushe kwamba bila kujali umri na tofauti zetu, sisi sote tumepewa karama tofauti tofauti ili tufanye huduma tofauti kwa ajili ya Bwana. Bwana wetu ni mmoja, na kupitia kwake tumefumwa pamoja kwa kusudi. Sisi kila mmoja ana uwezo wake, karama yake, uelewa wake, thamani yake, mawazo yake, nguvu na udhaifu wake, lakini tukija pamoja tunaweza kustawi katika Mungu na kutoa utukufu kwake Mungu mweza Baba wa Mbinguni katika Mwana wake Yesu, Bwana na Mwokozi wetu.

Baba yetu wa Mbinguni, twakushukuru kwa kutuchukua na kutufanya wako katika familia yako. Ingawa sisi ni viumbe wa kipekee, tunaotofautiana katika ujinsia, umri na karama, wewe unatujenga pamoja na kusudi, tusaidie tuone mapenzi na uzuri ulio ndani ya kila mmoja. Tunataka tusherehekee tofauti zetu kwa umoja tukiheshimiana na kupendana katika nyumba zetu, kanisani, katika jamii na katika sehemu zetu za kazi. Amina.

**KAPTENI DOROTHY CHRISTOPHER MACWAN**
INDIA MAGHARIBI

Mimi ni Kapteni Dorothy Christopher Macwan kwa sasa natumika kama katibu wa Rais wa Huduma ya Wanawake, naishi Mumbai. Mume wangu Kapteni Christopher A. Macwan anatumika kama Katibu wa teritori wa vijana wa Gujarat. Tunafurahia kumtumikia Bwana wetu katika daraja na maagizo tuliyopewa ndani ya Jeshi la Wokovu. Mungu atubariki sote. Amina.

*Toka wakati wa kuandika, Kapteni Dorothy amepata agizo jipya Makao Makuu ya Kimataifa, anakotumika kama Naibu Katibu wa Kanda ya Asia ya Kusini.*



# MAJI NDIYO HUTOA UHAI KWA VYOTE

YOHANA 4

MEJA CHRISTINE DE MAINE

‘Wakati mwanamke Msamaria alipokuja kuchota maji, Yesu alimwambia, “Nipe maji ninywe?” (Wanafunzi wake walikuwa wamekwenda mjini kununua chakula.) Mwanamke Msamaria akamwambia, “Imekuwaje wewe Myahudi kutaka maji kwangu, nami ni mwanamke Msamaria? ” (maana Wayahudi hawachangamani na Wasamaria.) Yesu akamjibu, “Kama ungaliijua karama ya Mungu, naye ni nani akuambiaye, nipe maji ninywe, ungalimwomba yeye, naye angalikupa maji yaliyo hai.”

Umewahi kunywa maji safi moja kwa moja kutoka kwenye chanzo chake badala ya kutoka bombani? Nimewahi kufanya hivyo na maji hayo yalikuwa matamu na yenye ladha nzuri. Unaweza kufikiria maji ya kutoka kwenye kisima cha Yakobo yangekuwa na ladha ya namna gani? Kisima cha Yakobo katika Yohana 4 kina ukweli wa kihistoria inayokwenda nyuma hadi Mwanzo 33 wakati Yakobo aliponunua ardhi hiyo na akaweka kambi. Ni wakati huu binti yake Yakobo aitwaye Dina ‘haki yake ilikiukwa’ na Shekemu mwana wa mtawala wa eneo, Hamori, Mhivi, kitu ambacho kilianzisha hasira kati ya Yakobo na wanae. Kwa huzuni, kwa wote waliohusika hii ilikuwa hali ambayo haikumalizika vizuri pande zote na Biblia haituelezi nini hatimaye kilifanyika kwa Dina. Miaka mamia baadaye, kisima hiki bado kinawahudumia wengi na kupitia kwa Yohana 4 tunaweza kusoma juu ya kukutana kati ya mwanamke Msamaria (ambaye Biblia haimtaji jina) na Yesu kisimani.


Yesu anafika kisimani na anawatuma wanafunzi wake waende mjini kununua vitu. Yuko peke yake na bila shaka anajisikia amechoka, ana kiu na anahitaji maji. Tunafahamu kwamba ilikuwa mchana katikati, na mwanamke Msamaria alikuja kuchota maji kwa ajili yake na nyumba yake. Katika hali ya wakati huu, Yesu na mwanamke huyu kabisa wasingekuwa na lolote la kufanya pamoja. Hawahesabiki kuwa wanalingana kwa sababu ya ujinsia wao, utaifa, utamaduni na hali yao katika jamii, na ninaamini alikuja kisimani mchana jua kali ili awakwepe watu.

## ‘YESU ANAMWONA MWANAMKE HUYU KUWA NI MTU MKAMILIFU NA ANAMPA UKOMBOZI NA UREJESHO.’

Hata hivyo, nafikiri Yesu alitambua kwamba yupo mahali sahihi, kwa wakati sahihi, na katika siku sahihi kwa mazungumzo haya kufanyika. Tunafahamu kwamba mwanamke Msamaria alishangazwa alipozungumza naye kwa sababu kwa haraka alieleza kwamba wao ni wa makabila tofauti na imani tofauti. Anafahamu kwamba Yesu ni Rabi Myahudi, mwanaume anayezungumza naye, na anayemwomba ampe maji kutoka kisimani anywe. Hata hivyo, Yesu kwa kuwa alivyo, hamwoni kuwa hana thamani kwa sababu ya imani na jinsia yake, au hamhukumu kwa sababu ya mambo yake ya huko nyuma, mambo ya nyuma ambayo ni pamoja na kuwa na wanaume wengi tofauti. Katika jamii ya mfumo dume, huyu mwanamke angekuwa na hadhi ndogo ya jamii. Yesu anamwona mwanamke aliyevunjika na anaweza kutimiza na ana njaa kubwa ya kiroho ambayo ni yeye tu anaweza kumtosheleza.

Sote tunahitaji maji yatudumishe, na maji ndiyo yanayotoa uhai kwa vitu vyote. Yesu anamwomba mwanamke Msamaria maji, na hazungumzii ‘maji yaliyo hai’. Mwanamke anaonekana kama hafahamu sawasawa anachoambiwa na Yesu, lakini Yesu akaanza kumfunulia mambo anayofahamu kuhusu maisha yake, naye akaanza kutambua kuna mengi zaidi yanaendelea hapa.

Maji ni chanzo cha thamani kwetu sisi sote na katika utamaduni wetu wa Māori, maji ni msingi wa maisha na ni kile kinachotuunganisha na ardhi na ushirika wetu nayo. Huko New Zealand, mara nyingi sisi hujitambulisha



## JADILI:

* Baada ya kusoma Yohana 4, maji yana maana gani kwako? Je, maji yana maana yoyote muhimu kwako?
* Unawezaje kuwakubali kikamilifu watu waliotofauti na wewe katika maisha yako?
* Yesu alikutana na wewe namna gani kisimani?

kwa pepeha. Ni salamu inayoanza na mlima muhimu na mto na mahali ambapo ni muhimu kwetu. Tunafanya hivyo kwa sababu sehemu hizo haziondoki zipo hapo siku zote. Kisima cha Yakobo ni aina hii ya mahali na kisima hiki kina kina kirefu na maji yanabakia yale yale kwa Dina kama yalivyo kwa mwanamke huyu. Hiki ndicho kisima kilicho muunganisha Yesu

Na akampa nafasi kumwambia huyu mwanamke Msamaria kwamba anaweza kunywa kutoka katika chanzo cha kiroho kilicho kikubwa zaidi ya kile alichokuwa anakifahamu. Ukabila wake ulikuwa umempa mawazo yasiyokamilika kuhusu Mungu, lakini Mungu anahamu naye na wengine wengi wanywe kutoka kwa kile ambacho Mungu anaweza kuwapa kupitia kwa Yesu Kristo. Kama 1 Wakorintho 13:5 isemavyo, upendo 'haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake, hauoni uchungu, hauhesabu mabaya.'

Mungu anamwona mwanamke huyu kuwa ni mtu mkamilifu na anampa ukombozi na urejesho. Inaonekana kama ni mwangwi kutoka siku za nyuma, kutoa urejesho kwa yale yaliyomtokea Dina katika kisima hiki miaka yote hiyo iliyopita. Wakati huu mwanamke Msamaria aujia uzima wakati Yesu alipojitambulisha kwamba yeye ni 'Masihi (anayeitwa Kristo)'. Arudi mjini kuwaambia watu, 'Njoni mtazame mtu ambaye ameniambia mambo yote niliyoyatenda. Je haimkini huyu kuwa ndiye Kristo?'

Tofauti ya Dina na familia yake, kukutana huku kunaleta maisha mapya mahali palipokuwa na mauti. Tunaona duara kamili la jinsi Mungu anavyofanya kazi kwa kurudia – katika maneno yake na katika maisha ya watu katika historia nzima – wengi wao tunaowasoma katika Biblia ambao sasa tunajifunza na kuwasoma. Katika Yohana 4, mwanamke huyo akaenda na kuwashawishi Wasamaria wengine wengi wawe tayari kusikia na kumpokea Yesu. Sasa mwanamke huyu anakwenda kutoka kuwa aliyekataliwa katika mji wake hadi kuwa aliyerejeshwa, aliyeponywa, aliyeamini na kuongoza jamii yake kwenye maji yaliyo hai yanayotolewa na Yesu. Ukombozi unawasili kwenye jamii nzima na kwenye historia ya kisima hiki, inadaiwa na uponyaji kupitia kwa kukutana huku. Mambo yasiyo ya haki ya huko nyuma sasa ni duara kamilifu la upatanisho na urejesho ambao ni Mungu tu angeweza kuuleta kupitia kwa mwana wake Yesu Kristo.

Hii ni hadithi maridadi ya ukombozi. Mwanamke Msamaria anarejeshwa kwenye uzima kupitia kwa 'maji yaliyo hai' ya Yesu. Sio tu kwamba maji haya yatakasayo yanamkomboa na kuponya hali yake, lakini yanaponya vile vile vidonda vyake vya zamani vilivyoachwa na yale yaliyofanywa kwa Dina. Inatukumbusha kwamba siku zote Yesu alikuwa akihusika na uponyaji wa wanaokandamizwa na kuwaweka sawa wasio na haki. Kwa vifo tunavyopitia, Yesu hutusafisha kwa maji yaliyo hai – na sio tu kwa ajili yetu lakini yapo kwa ajili ya kuwashirikisha wengine. Kisima cha uzima hakikauki.



Baba, tusaidie kupenda, kuwakubali na kuwakaribisha wengine kama ufanyavyo wewe. Twaomba tuwasambazie maji yaliyo hai wale wanaokuhitaji lakini hawakujui. Amina.

**MEJA CHRISTINE DE MAINE**
NEW ZEALAND, FIJI, TONGA NA SAMOA



Tēnā koutou katoa Ko Christine ahau Nō Aotearoa ahau Salamu kwenu nyote. Mimi ni Christine kutoka New Zealand. Nimekuwa afisa wa Jeshi la Wokovu kwa miaka 17 na nimeolewa na nina wavulana wawili. Napenda kuwa na familia yangu na marafiki. Napenda kujifunza kuhusu mila zetu za kuwa Māori na kujifunza kuongea lugha yetu.

# KUWAZUNGUMZIA WATU WENYE ULEMAVU

MITHALI 31:8-9

CORALIE BRIDLE

William Booth akiwa mgonjwa amelala na hajiwezi wakati neno lake moja maarufu la simu ya maneno liliwahimiza waumini wa Jeshi la Wokovu wawafikirie 'wengine'. Zaidi ya miaka mia moja baadaye, inaweza kusisitiziwa kwamba dunia inaweza kuwa mahali pazuri zaidi kama tungekuwa makini zaidi kwa uhamasishaji wake. Vile vile vifungu hivi katika Mithali 31 haraka vyatusukuma kuchukua hatua maalum kwa niaba ya wengine – kuwazungumzia, kuhukumu kwa haki na kutetea haki za wengine. Hekima ya Mithali inaelekeza kwenye maarifa yetu na mwenendo wetu. Hiyo, haitoshi kufahamu kwa nadharia tu tunatakiwa kufanya namna gani. Mithali inatuhimiza kutenda kufuatana na maarifa hayo.[1]

Maelekezo yanayopatikana katika vifungu hivi kwa asili ni ujumbe kutoka kwa mama kwenda kwa mvulana wake. Kama mfalme, mtoto ana uwezo mkubwa sana na wajibu. Mama yake anamwelekeza atumie sauti yake kuwazungumzia wengine. Utambulisho halisi wa mfalme haujulikani. Hapa anajulikana kama Lemuel, lakini wasomi wamegawanyika juu ya huenda maneno haya yanamhusu Mfalme Sulemani na mama yake Bersheba, au labda Lemuel anaweza kuwa alikuwa ndiye Mfalme wa Massa, mmoja wa wazao wa Ishmaeli.[2] Leo tunaweza tusijikute tuna nafasi za mama malkia au mfalme, lakini kama warithi wa utamaduni, maelekezo ya vifungu hivi yanazungumza kupita muda na tamaduni zote.

Kuzungumzia wengine sio kila mara ni hatua ya moja kwa moja. Nakumbuka daktari mwenye huruma aliwahi kumalizia uchunguzi wa afya ya mvulana wangu na akasema kwamba 'itabidi tumsubiri yeye mwenyewe aiseme hadithi yake mwenyewe'. Hata hivyo, ulemavu wa mwanangu ulimfanya ashindwe kuelezea hadithi yake au kwa kweli ajieleze kwa njia nyepesi inayotambulika. Kumzungumzia, kama alivyoishi maisha yake na ulemavu mkubwa, kumekuza wajibu wa *utetezi wa zile tofauti ndogo*. Natumia maneno haya *zile tofauti ndogo* kwa makusudi kwa sababu utetezi kwa niaba ya wengine unahitajika kufanywa kwa makubaliano makini.

Kufuatilia utetezi wa zile tofauti ndogo kunahitaji tuhakikishe kwamba kuwazungumzia wengine hakubadiliki na kuwa *kuzungumza kwa niaba* au *kuzungumza juu ya* mtu mwenye ulemavu. Mwelekeo wa namna hii hauungi mkono na hudhalilisha. Tafsiri ya neno 'maskini' katika maandishi yetu lina wazo la 'kutoweka'. Maskini ni wale ambao watoweka kutoka katika akili zetu, ajenda zetu au kutoka katika kusanyiko letu, kwa sababu sisi tumewatowesha waende pembezoni mwa jamii zetu. Kama hatuko makini na hatuna habari, kumzungumzia mwenye ulemavu kunaweza kusababisha atoweke zaidi. Kumtendea kila mmoja sawasawa sio utafutaji wa usawa. Mazingira mbalimbali, uzoefu na utamaduni vinaitisha pawepo na umakini katika ufundi wa kuwazungumzia wengine. Hii inahitaji muda, usikivu, kutengeneza urafiki na uwazi katika kujifunza njia mpya na mbalimbali za kuingiana na wengine.

Kinyume na Mfalme Lemuel wewe haitawezekana kukaa katika kiti cha ufalme ukitoa hukumu juu ya mambo ya taifa. Hata hivyo, unaweza kuwa unatoa hukumu juu ya watu wenye ulemavu wanaopuuzwa, pasipo haki au bila ufahamu mzuri. Kudhania watu siku zote ni hatari kubwa. Huharibu jinsi tunavyoiona sura ya Mungu ikidhihirika katika uso na hali iliyo mbele yetu. Kuzungumza kwa ujumla, watu wanaoishi na ulemavu kwa kweli wanataka kuishi maisha ya kawaida. Wanataka wakubalike kama walivyo. Wanataka kusherehekea maisha. Wanataka kushiriki katika furaha ya maisha na kuabudu pamoja na wengine wanaotaka kufanya vivyo.


Mfalme katika maneno aliyopewa alitakiwa kulinda haki za maskini. Wastani wa asilimia 15% ya idadi ya watu wanaishi na ulemavu wa aina fulani. Duniani kote wanaendelea kukabiliana na kukosa haki, kukandamizwa, kubaguliwa na kunyanyapaliwa. Kitakwimu wao kiuchumi wametengwa, wanakabiliana na viwango vya juu vya wasio na kazi na wanateseka kwa vifo vya mapema ukilinganisha na watu wasio na ulemavu. Kutetea utu wao na haki yao kama binadamu ambao Kristo aliwafia ni jukumu muhimu kwa Jeshi la Wokovu duniani.[3]

---

1 R Murphy and E Huwiler, New International Biblical Commentary: Proverbs, Ecclesiastes, Song of Songs (Peabody, Massachusetts: Hendrickson, 1999), 7.

2 Katharine J. Dell, The Book of Proverbs in Social and Theological Context (Cambridge: Cambridge University Press, 2006), 82.

3 The Salvation Army, International Positional Statement: Disabilities (London: International Headquarters, 2020



## JADILI:

* Dhana ya utetezi wa zile tofauti ndogo unaweza kuathiri namna gani ninavyozungumza na kutenda kwa niaba ya wengine?
* Ni kwa njia zipi naweza kushawishi mienendo ya jamii kwa watu wenye ulemavu ili waweze kuendana na ukweli wa injili?
* Hao watu ‘wengine’ katika agizo langu la sasa ni watu gani, au maeneo ya huduma ni yapi, wanaohitaji kutiwa moyo nami au wanaohitaji sauti yangu leo?

Katika maisha yao, Catherine na William Booth walikutana kibinafsi na ufahamu wa dunia yenye ulemavu. Mmoja wa mabinti zao, Marian, alikuwa mgonjwa sana alipokuwa mtoto mdogo na ikasababisha aishi na kile tunachoweza kukiita leo ulemavu unaoendelea. Wakati Catherine alikiri wazi ana kiwango fulani cha huzuni kinachosababishwa na hali ya Marian, Marian mwenyewe hakufichwa. Katika umri ambao walemavu wengi hupelekwa kwenye taasisi – hii ilikuwa namna ya kuwazungumzia watu wengine wenye ulemavu. Umbo dhaifu la Marian lilijulikana kwa waumini wa Jeshi la Wokovu wa kipindi hicho.[4] William na Catherine waliona zaidi ya mapungufu yaliyojitokeza na wakamwezesha Marian kuishi maisha ya kawaida ilivyowezekana.

**‘KUFUATILIA UTETEZI WA ZILE TOFAUTI NDOGO KUNAHITAJI TUHAKIKISHE KWAMBA KUWAZUNGUMZIA WENGINE HAKUBADILIKI NA KUWA *KUZUNGUMZA* KWA NIABA AU *KUZUNGUMZA* JUU YA MTU MWENYE ULEMAVU.’**

Mwana theolojia Colin Gunton aliandika, ‘Sio ajali ya bahati mbaya bali ni utukufu wetu kwamba sisi ni wengine: kila mmoja wa kipekee na wa tofauti.’[5] Kwamba sisi ni tofauti na wengine ni jambo la kusherehekea. Hatutaki kile *kingine* cha wengine kitoweke, au sisi tuwe mwili wenye utupu, uendeshwao kama mtambo, wenye kufanana. Tofauti ni sehemu ya uumbaji wa Mungu. Kuwazungumzia wengine, kutetea haki zao na kuhukumu kwa haki, kukamilisha mwito wa kutenda, huheshimu utambulisho wa kipekee na kupasisha wito wa William Booth wa kuwakumbuka wengine.

---

4 John Larsson, Those Incredible Booths (London: Salvation Books, 2015), 241.
5 Colin Gunton, The One, the Three, and the Many: God, Creation, and the Culture of Modernity (Cambridge: Cambridge University Press, 1993), 196.

Baba wa Mbinguni, nifinyange mimi niwe mwanamke aliye wazi kupokea neema iliyofunuliwa katika watu wanaoishi na ulemavu.

### CORALIE BRIDLE

NEW ZEALAND, FIJI, TONGA NA SAMOA



Coralie ni mwanafunzi wa Yesu Kristo, muumini wa Jeshi la Wokovu wa maisha na anahudhuria kikao cha Auckland City huko New Zealand. Uuguzi wa magonjwa ya saratani ndiyo uti wa mgongo wa kazi yake. Mume wake, Kevin, watoto watatu watu wazima na wajukuu wawili, kunamfanya atulie katikati ya mambo ya maisha ya sasa. Yeye anahudumu katika Baraza la maswala ya Maadili na Jamii huko New Zealand na kwenye Baraza la Kimataifa la Theolojia. Coralie kwa sasa anashughulikia kupata shahada inayohusu kuangalia jinsi Jeshi la Wokovu linavyo wasaidia watu wenye ulemavu mkubwa katika makusanyiko New Zealand.

# NCHA YA BARAFU

HESABU 12:1-16

KAPTENI ESTHELA SANIZACA

Unaweza kuwa umeona barafu ya baharini. Kinacho nishangaza mimi kuhusu barafu hizi kubwa baharini ni kwamba kile unachokiona juu hakifanani na ukubwa wake halisi kwani sehemu kubwa imo ndani ya maji.

Katika Hesabu 12, tunakutana na hadithi ya Musa na ndugu zake wawili, Haruni na Miriamu. Tunafahamu kwamba Musa alikuwa kiongozi aliyechaguliwa na Mungu awaongoze watu wake, Waisraeli. Haruni alikuwa kuhani mkuu na Miriamu alikuwa mkubwa na nabii wa kike.

Miriamu alikuwa wa muhimu sana kwa maisha ya Musa toka alipokuwa mtoto (Kutoka 2). Katika Kutoka15:20-21 tunasoma kwamba aliongoza kuimba wimbo mzuri wa ushindi wa imani na shukurani alipoona tendo kuu la Mungu. Hata hivyo, baadaye tunamkuta akiongoza, pamoja na Haruni, tendo la upinzani dhidi ya Musa kwa sababu ya mkewe, Mkushi.

Kush lilikuwa jimbo kaskazini ya Misri lililojulikana kuwa la watu wenye ngozi nyeusi na wasomi wanaamini kwamba inawezekana mke wa Musa alikuwa na ngozi nyeusi.

Manung'uniko ya Miriamu yanaweza kuwa yalihusu Musa kuoa mke wa taifa na rangi nyingine. Lakini hii ilikuwa ni 'ncha ya barafu', kwani chini ya masengenyo na kutomkubali kuwa mke wa Musa, palikuwa na kujikweza sana na tatizo la wivu. Kukataliwa na ukosoaji wa wengine hudhihirisha jambo lililo na kina linaloendelea moyoni.

'"Mungu ameongea kupitia kwa Musa peke yake?" waliuliza. "Hajaongea kupitia kwetu vile vile?"'


**'MUNGU ANAENDELEA KUONYESHA WEMA WAKE KWA KUTUITA KWENYE MSAMAHA NA UPENDO WA DHATI MMOJA KWA MWINGINE.'**

Kifungu hiki kinatuonyesha wazi sababu halisi ya Miriamu kuonyesha tabia ya dharau na masengenyo. Wote Miriamu na Haruni walikuwa wamepokea karama tofauti kutoka kwa Bwana wazitumie kumtumikia yeye na watu wake, lakini inaonekana kama hii haikutosha. Walijisikia ni jasiri wa kutosha katika uwezo wa kutumika sawa au hata zaidi ya Musa. Hakuna linalotosheleza kwa moyo wa kujikweza.

Kifungu hiki kinaendelea: 'Bwana alisikia walichokisema.' Hakuna aliyemwambia! Alisikia kile ambacho Miriamu na Haruni walikisema. Alisikia kila neno walilolisema na alifahamu kusudi lililokuwa ndani ya mioyo yao.

Kwa mkono mmoja, kila jambo linamwelekea Miriamu kuwa ndiye chanzo wa upinzani huu, lakini hebu tusimpoteze Haruni. Haruni anaonekana kuwa mwepesi sana kuvutwa kwenye madai mengine. Kwa upande mwingine, tunamwona akishawishika kufanya mambo ambayo aliyafahamu kuwa sio sahihi, kama vile kuwakubalia Waisraeli kutengeneza ndama wa dhahabu (Kutoka 32). Katika wakati huu, tunaona akiegemea kwenye ushawishi wa dada yake Miriamu.

Kifungu cha 4 hadi 16 vinatuambia kuhusu matokeo ya matendo yao. Hakuna shaka kwamba Mungu hupinga kujikweza; katika swala la Miriamu, aliadhibiwa vikali. Hebu tukumbuke aliyoyasema Yesu: 'Kwa maana kila ajikwezaye atadhiliwa, naye ajidhiliye atakwezwa' (Luke 14:11).



## JADILI:

* Matendo yapi hudhihirisha uaminifu wa moyo wako?
* Je, wewe unashawishika kirahisi kuwadharau wengine?

Katika kifungu cha 13 Musa anakuwa mwombezi wa dada yake Miriamu kwa Bwana, na kama Mungu alivyomsamehe Miriamu na Haruni, Mungu anaendelea kuonyesha wema wake kwa kutuita sisi tutubu na tuwe na upendo wa dhati kwa wengine.

Umewahi kujiuliza ni jinsi gani watu wengine wanaiona imani yako katika Bwana? Je, moyo unaompenda Mungu na jirani yake unafananaje? Unaweza kuona jinsi moyo wenye kiburi unavyojifunua? Hii hudhihirisha kukataliwa, dharau na ubora zaidi ya wengine, walioumbwa kwa mfano na sura ya Mungu, kama wewe.



Bwana, twaomba utusafishe dhambi zetu na kujikweza kwetu katika hali zake zote. Wewe unalaani haya. Tafadhali tusaidie tukue katika upendo mmoja kwa mwingine. Kama ulivyotupenda, tufundishe kupenda. Amina.

**KAPTENI ESTHELA SANIZACA**

UHISPANIA NA URENO

Naishi kwa furaha nikiwa nimeolewa na Kapteni Franklin Sánchez na tuna mabinti wawili wazuri, Salomé na Ana. Nafurahia muziki na kusoma. Nimeitwa kutumika kwa neema ya Bwana. Kwa hivi sasa, natumika kama afisa wa kikao cha Las Palmas nami ndiye afisa wa vijana hapa Uhispania.



# UPENDO UNAOKOMBOA

HOSEA 3

LUTENI KANALI EVA DANSO

Hosea 3 ni sura fupi mno inayowaelezea Waisraeli uhamishoni na kurudi nyumbani. Waisraeli walipitia muda wa kusafishwa katika nchi ya kigeni, lakini Mungu bado aliwapenda watu naye alikuwa tayari kuwapokea mara tena. Mungu alimwamuru Hosea aonyeshe roho ya upendo huo huo na msamaha kwa mkewe, Gomeri. Ingawa Hosea alikuwa na sababu nzuri za kumpa talaka Gomeri, aliambiwa amnunue arudi na ampende kahaba na mke asiye tayari kutubu.

'Upendo' ni neno ambalo mara kwa mara linatumika. 'Napenda chokoleti', 'Napenda kikundi hicho cha michezo', 'Nampenda mwenzi wangu'. Ni mara kwa mara sisi 'hupenda' vitu! Lakini hili hubadilisha namna gani madai ya 'Mungu ni pendo' au 'Mungu ananipenda mimi'? Upendo unatakiwa kuwa wa pande mbili, lakini kwa upande wa Mungu, ulikuwa wa upande mmoja (Warumi 5:8). Mungu ni pendo, naye anataka watoto wake waonyeshane upendo.

Mungu wetu siku zote yupo kusamehe. Wana wa Israeli walitawanyika, lakini Mungu alikuwepo kuwasamehe walipomrudia. Anaendelea kutupenda hata tunapokuwa tumemkosea, naye huangalia kupita makosa yetu na hutupenda bila masharti (1 Yohana 4:9-12).

Mungu anatarajia tuuonyeshe upendo wa aina hii katika maisha yetu ya kila siku na mahusiano na watu wengine (1 Wathesalonike 3:11-13). Tunapoudhihirisha upendo wake tunakua katika utakatifu na tunakua tukifanana zaidi na Kristo. Katika nyumba zetu, tunawapenda namna gani wenzi wetu? Ule upendo wa kwanza uko wapi? Mara ya mwisho kuwastaajabisha wenzi wetu kwa zawadi, barua au ujumbe wa upendo ilikuwa lini? Mnasameheana kiasi gani? Unamwombea mwenzi wako kiasi gani?

Katika Hosea 3, Mungu anatuambia tuwaonyeshe upendo wenzi wetu na tusidumu katika kutenda mabaya. Badala yake tusamehe, tuwaombee wenzi wetu na tuombe Mungu aingilie kati. Katika Yohana 15:12 tunasoma: 'Amri yangu ndiyo hii, mpendane kama nilivyowapenda ninyi.'


Upendo ni msingi kwa Wakristo wote; tumeitwa kuwapenda majirani zetu kama tunavyojipenda wenyewe.

Kama mwana mpotevu, hebu tuonyeshe kujutia na turudi kwa baba yetu. Yeye yuko tayari kutukubali tena na kuturejesha upya.

Maelezo mazuri ya upendo yanapatikana katika 1 Wakorintho 13:4-8. Inatoa uelewa wa wazi wa nini maana ya upendo:

- Upendo huvumilia, hufadhili, upendo hauhusudu, upendo hautakabari, haujivuni.
- Haukosi kuwa na adabu, hautafuti mambo yake, hauoni uchungu, hauhesabu mabaya.
- Haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli.
- Huvumilia yote, huamini yote, hutumaini yote hustahimili yote.
- Upendo haupungui neno wakati wowote, bali ukiwepo unabii utabatilika, zikiwapo lugha, zitakoma, yakiwapo maarifa yatabatilika.

Upendo wetu kwa wenzetu unatakiwa kuonekana katika matendo yetu. Wakati mwingine watu tunaowapenda hawawezi kutupenda kama tunavyotaka watupende, lakini wakati wote kumbuka Warumi 5:8 'Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu tulipokuwa tungali wenye dhambi.'



**JADILI:**

* Ni mambo gani yanayozuia upendo wa kweli katika familia na kanisa letu?
* Tunawezaje kuendelea kuwapenda watu licha ya kushindwa kwao au kukataa kwao kurudisha upendo wa namna hii?
* Je, tukate tamaa kabisa ya kupendana?

Tulipokuwa tunatanga tanga mbali na Kristo, yeye alikuwa bado yupo hapo akionyesha upendo wake kwetu. Yohana 3:16 inatuambia: 'Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminie asipotee bali awe na uzima wa milele.' Huu ni upendo kazini; Mungu alimtuma mwanawe wa pekee kufa kwa ajili yetu.

## 'MUNGU NI PENDO, NAYE ANATAKA WATOTO WAKE WAONYESHE UPENDO KWA WENGINE.'

'Wapendwa natupendane, kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu, na kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu. Yeye asiyependa hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni upendo. Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma mwanawe pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa yeye.' (1 Yohana 4:7-9).

Mpendwa dada katika Kristo, katika shughuli zetu za kila siku, acha watu waone pendo ambalo Kristo ametupa likionekana kwa wengine; upendo utakaolainisha kila huzuni, upendo utakaofanya kila mzigo uwe mwepesi, upendo ambao hauna maswali na upendo ambao utashinda.

Mpendwa Bwana, tupe moyo wa upendo na utusaidie kuwapenda wengine kama tunavyojipenda wenyewe. Tusaidie kuvumilia na tusikate tamaa kuhusu watu tunaotakiwa kuwapenda, na kwamba jina lako litatukuzwa katika mahusiano yetu yote. Tunakushukuru katika jina la Yesu Kristo. Amina.

**LUTENI KANALI EVA DANSO**
NIGERIA
Luteni Kanali Eva ni Mkristo aliyejitoa na aliye tawazwa kuwa afisa wa Jeshi la Wokovu Ogasti 1991. Yuko katika ndoa na Isaac kwa furaha na wamebarikiwa na watoto watano na wajukuu 10. Ametumika Ghana na Makao Makuu ya Kimataifa. Sasa hivi anatumika kama Katibu wa Teritori wa Huduma za Wanawake Ghana.



# NABII WA KIKE ALIYECHAGULIWA NA MUNGU

## 2 WAFALME 22:14-20; 2 MAMBO YA NYAKATI 34:22-33

MEJA EVAMA SHAIJURAJ

'Siku ile Mungu aliumba mtu, kwa sura ya Mungu alimfanya; mwanamume na mwanamke aliwaumba, akawabariki..' (Mwanzo 5:1-2).

- Biblia inatoa msaada wa usawa wa wanaume na wanawake katika uumbaji na katika ukombozi, na inafundisha wanawake na wanaume waliumbwa kwa mfano wa Mungu kwa ajili ya ushirika kamili wa usawa (Mwanzo 1:26-28, 2:23; 1 Wakorintho 11:11-12; Wagalatia 3:28).

- Biblia inatwambia kwamba Yesu Kristo alikuja kuwakomboa wanawake na wanaume: 'Kwa imani sote twafanywa watoto wa Mungu katika Kristo na warithi wa Baraka za wokovu' (Warumi 8:14-17; vile vile Yohana 1:12-13; Wagalatia 3:26-28).

- Biblia inasema Roho Mtakatifu aliwajia wanaume na wanawake wakati wa Pentekoste bila kutofautisha na anaishi ndani yao na anagawa karama bila kujali jinsia (Matendo 2:1-21; 1 Wakorintho 12:7, 14:31).


- Biblia inaonyesha kwamba wanaume na wanawake ni warithi wa neema ya uzima na wafungwa pamoja katika uhusiano wa kujitoa kwa pande zote na wajibu (Waefeso 5:21; 1 Petro 3:1-17).

Katika Agano Jipya na Agano la Kale, wanaume na wanawake wote wanatoa huduma ya unabii, uchungaji na huduma za kifalme. Manabii wa kiume na wa kike wametajwa kote katika maagano yote. Neno zoefu linalotumika kwa nabii wa kiume au mzungumzaji ni 'Nabii' Kiebrania. 'Nebiah' ndilo jina linalotumika kwa nabii wa kike. Nabii wa kiume au nabii wa kike ni mdomo wa Mungu, ni mwombezi na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu. Katika utamaduni wa Manabii, walikuwepo manabii wa Kiebrania 48, manabii saba wa mataifa na saba manabii wa kike: Miriam, Debora, Hulda, Sara, Hanna, Abigaeli na Esta.

Hulda alikuwa nabii wa kike aliyejitoa, aliyeheshimiwa na aliyejulikana sana katika Israeli wakati wa mfalme Yosia. Alikuwa mke wa Shallum – mjomba wake nabii Yeremia – na aliishi katika jengo jipya Yerusalemu. Jina 'Hulda' lilitokana na neno la Kiebrania 'lemma', 'kukaa' au 'kuendelea'. Maana nyingine ni 'mnyama mdogo'. Jina lake linatajwa katika 2 Wafalme 22:14-20 na 2 Mambo ya Nyakati 34:22-28. Ingawa ni sehemu ndogo ya neno zima la Mungu, linaheshimiwa sana. Alileta ujumbe kwa mfalme kutoka kwa Mungu. Kufuatana na William E. Phipps, profesa wa dini na filosofia, Hulda ni mtu wa kwanza kutangaza maandishi fulani kuwa ni matakatifu. Rabi walipewa heshima kubwa, waliotangaza kuhusu ukuta wa magharibi, lango la Makuhani na lango la Hilda haikutakiwa kuharibiwa. Inasemekana kwamba ni makaburi ya Mfalme Daudi na Hilda ndiyo yaliyoruhusiwa kuwa ndani ya Yerusalemu. Licha ya ubaguzi ambao wanawake walikabiliana nao wakati huo, Mungu alimchagua Hulda na manabii wengine wanawake kote katika Agano la kale na Agano Jipya ili kwa mamlaka walete Neno lake kwa watu wake.

Mfalme Yoashi alichaguliwa na Mungu afanye ukarabati wa hekalu na alete uamsho mkubwa. Wakati wa ukarabati wa hekalu, Hilkia kuhani alifanya uvumbuzi mkubwa: 'Kitabu cha sheria cha Bwana kilichotolewa kupitia kwa Musa' (2 Mambo ya Nyakati 34:14). Alimpa kitabu hicho Shafani Mwandishi. Shafani alimsomea kitabu hicho Mfalme, na Mfalme aliposikia maneno ya kitabu cha sheria alichana joho lake na akampa amri hizi Hilkia: 'Nendeni mkamuulize Bwana kwa ajili yangu, na kwa ajili ya watu hawa, na kwa ajili ya Yuda yote, katika habari za maneno ya kitabu hiki kilichoonekana; kwa kuwa hasira ya Bwana ni kubwa aliyotukasirikia, kwa sababu babu zetu hawakuyaangalia maneno ya kitabu hiki, kuyafanya kama hayo yote tuliyoandikiwa.' (2 Wafalme 22:13).

Ni kwa njia ipi kuhani mkuu na watu wake wamuulize Bwana? Nani atakuwa mtafsiri mzuri wa akili zake? Hakuwepo kuhani mkuu kuliko Hilkia. Shafani inawezekana alisimama juu ya waandishi. Lakini wote Hilkia na Shafani walitambua kwamba kuna mmoja Yerusalemu aliye na uelewa wa Mungu mzuri zaidi. Nabii wa kike! Walimuuliza Hulda kama kilikuwa kitabu cha kweli cha Mungu. Hulda akathibitisha hilo Ilikuwa Neno



## JADILI:

* Unaona sifa zipi ndani ya Hulda?
* Uko tayari kuwa kiongozi kama Hulda na uzungumze Neno la kuzaliwa upya na mabadiliko kwenye jamii yako?
* Ushirika wako na Bwana ukoje? Kama mwanamke wa Mungu, uko tayari kupokea ujumbe wake kwa watu wake?

la Mungu na watu na mfalme waliokubali tamko lake – ilikuwa ni njia ya hukumu na njia ya wokovu. Mfalme na watu wake wakafanya upya imani yao, ikasababisha kiapo cha taifa cha kumfuata Mungu wa mababu zao kwa uaminifu.

Sifa za kipekee za uongozi wa Hulda:

- Hulda hakuwa mwoga kuzungumza kwa ujasiri ukweli, kwa uadilifu.
- Watu walikwenda kwake kwa sababu ya jinsi alivyoishi – alikuwa mfano mzuri.
- Alichukuliwa kwa heshima kubwa na watu wa kawaida na hata wafalme.
- Alikuwa na ushirika endelevu na Bwana wake.
- Aliitwa wakati wa matatizo – kinachoelezea kwamba alionekana kuwa kiongozi.
- Mwanamke huyu alikuwa nabii kipindi kile kile cha Yeremia na Sefania – lakini kilichotafutwa kwake kilikuwa ushauri wake.
- Hakuzungumza kwa mamlaka ya kwake binafsi, alizungumza kama mjumbe wa Mungu tu.

## ‘WANAWAKE NA WANAUME WALIUMBWA KWA MFANO WA MUNGU KWA AJILI YA USHIRIKIANO KAMILI NA ULIO SAWA.’

Hulda alikamilisha huduma yake; ni baraka na nafasi ya upendeleo kutumiwa na Mungu kwa ajili ya kusudi lake! Twaomba Mungu ainue akina Hulda wengi katika kizazi hiki kwa ajili ya matengenezo na kuwekwa wakfu kwa watu wetu na taifa letu.

Mpendwa Mungu, kama mtoto wako, tafadhali nisaidie nikusogelee kupitia kwa nafasi ya upendeleo ya ushirika nawe nipokee neno lako ili niweze kwa ujasiri kulitangaza kwa kizazi cha watu wangu. Katika jina la Yesu, amina!

**MEJA EVAMA SHAIJURAJ**
INDIA MAKAO MAKUU YA TAIFA
Mimi ni Mhariri wa ofisi ya taifa la India huko Kolkata. Mume wangu Meja Shaijuraj ni Afisa Mkuu wa Fedha. Tumekamilisha miaka 22 katika huduma ya Bwana, naye ni mwaminifu! Tuna mtoto wa kiume, Shiljo (21) na msichana, Riya (18).



# KUMHESHIMU KRISTO KATIKA MAHUSIANO YETU

1 PETRO 3:8-9

LUTENI KANALI JANET ASHCRAFT

Afya njema ya akili inahitaji mawasiliano na watu wengine. Moja ya mafunuo ya kwanza ya Biblia ni kwamba Mungu alituumba kwa namna ambayo tunawahitaji watu wengine: 'Si vema huyo mtu awe peke yake' (Mwanzo 2:18). Mahitaji mawili ya msingi sana na ya muhimu kweli tuliyo nayo ni upendo na kukubalika katika jamii. Haya hutupeleka kwenye maisha yanayoshamiri ambayo ndiyo hamu ya Mungu kwa kila mmoja. Katika Maandiko maelekezo mengi tunayokutana nayo, yakiwekwa katika matendo, huongoza kuelekea kwenye maisha yanayoshamiri kiakili, kimwili na kiroho. Neno la Mungu huburudisha nafsi, humfanya mtu wa kawaida awe na hekima na huleta furaha moyoni (Zaburi 19:7-8). Katika Agano jipya tunaweza kuona umuhimu unaowekwa juu ya uhusiano na jinsi tunavyotakiwa kuwatendea wengine. Katika 1 Petro 3:8-9 tunaona maelekezo yaliyo muhimu kwa muundo wa afya ya akili, na maisha yanayoshamiri ambayo Mungu anataka kila mmoja awe nayo.


1 Petro inaelekezwa kwa kikundi cha watu ambao walikuwa wa Mataifa na wakatoroka nyumbani kwa sababu ya kuteswa kwa sababu ya imani yao kwa Yesu. Imejaa mambo ya kutia moyo na maelekezo ya jinsi ya kuishi na kuwatendea wengine ili Kristo aheshimiwe. Kabla ya 1 Petro 3:8, Petro aliandika juu ya jinsi tunavyotakiwa kuishi kwa mahusiano na makundi maalum. Kuanzia mstari wa 8 Petro anatoa muhtasari wa yale yote aliyoyasema mapema, akiangazia sifa zinazotakiwa kuonekana katika mahusiano yetu yote na wengine. Kila thamani inasababisha afya njema ya akili sio tu kwetu sisi, lakini vile vile kwa wale tunaohusiana nao yanapowekwa katika matendo. Ni muhimu kwetu kuziona sifa hizi zinazopatikana katika mstari wa 8 kwamba sio tu mapendekezo – ni maelekezo imara: '**Hatimaye, nyote…**'

**'…mpatane nia zenu.'** Hii inaelekeza kwenye umoja juu ya mambo makuu yanayohusu imani ya Wakristo kati ya waamini. Vipengele muhimu vya imani ya Kikristo vinaelezwa katika imani ya Mitume. Haina maana kukubaliana katika mambo yote, lakini ina maanisha tuanzie mahala pamoja pa kuanzia. Bado tutakuwa na tofauti za kweli na nzito, lakini umoja unaopatikana katika Yesu lazima uzidi zile tofauti. Tunatakiwa kufanya kwa bidii tusiruhusu tofauti za mawazo zisababishe kuvunjika kwa mahusiano. Tunaona huu umoja, unaofanana kimawazo, ukifafanuliwa katika Matendo 2:1: 'Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwa wote mahali pamoja,' na Warumi 12:16: 'Mpatane nia zenu ninyi kwa ninyi.'

**'UMOJA UNAOPATIKANA KATIKA YESU LAZIMA UZIDI ZILE TOFAUTI.'**

**'…muwe na huruma.'** Neno hili 'muwe na huruma' linatokana na maneno mawili ya Kiyunani, moja ambalo linamaanisha 'kuathirika' na kitu – kujisikia; na jingine ni 'pamoja', kwa hiyo ni 'kujisikia pamoja'. Inaelezea kubadilishana hisia na mwingine, iwe ni furaha au huzuni. Tunayaona haya katika Warumi 12:15: 'Furahi pamoja nao wafurahio, lieni pamoja nao waliao.' Unapokuwa una huruma na mtu, utafahamu kinachoendelea katika maisha ya mwenzio, na uko tayari kuwa katika mahusiano ya kutoa na kupokea.

**'…mpendane.'** Mpendane kama kaka na dada. Watu wanaopendana. Upendo wa jinsi hii 'upendo' ni sawa na katika 1 Petro 1:22, inayosema, 'jitahidini kupendana kwa moyo'. Ni mapenzi yaliyo ya dhati na ya ndani. Kama inavyowekwa na masomo ya Agano Jipya ya *Wuest*, 'ni upendo wa kupenda'. Hii ndiyo aina ya upendo ambao Yesu aliuzungumzia katika Yohana 13:35, 'Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.'



## JADILI:

* Ni kipi unachokiona ni kigumu kukiweka katika mazoezi kutoka vifungu vya 8-9? Kwa nini?
* Je, inawezekana kuishi kikamilifu kwa njia hii bila ya msaada wa Roho Mtakatifu?
* Mwingiliano sahihi wa jamii hulea huruma, imani na ukaribu na wengine. Vile vile husaidia kuepusha msongo wa mawazo na huzuni. Washirikishe wengine kuhusu wakati ulipitia hili.

**'...wenye kuelewa (huruma).'** Hii ni kuwa na mioyo laini mmoja na mwingine, hasa wanapokuwa wanateseka. Ni kinyume cha mioyo migumu, kinachoweza kutendeka kwa mioyo yetu wakati fulani kwa maumivu ya mwingine. Tunapokuwa tumepitia magumu na mateso sisi wenyewe inakuwa rahisi kuwaelewa wengine. Mwanzilishi wa World Vision International, Bob Pierce, alisema 'Acha moyo wangu uvunjike na mambo yanayouvunja moyo wa Mungu.'

**'...[uwe] mnyenyekevu.'** Kuwa mnyenyekevu sio sawa na kutojithamini. Ni kuyatizama maslahi ya wengine zaidi ya yale ya kwako. 'Uvumilivu wa kweli sio kujifikiria wewe ni wa chini, ni kujifikiria kidogo' (C.S. Lewis). Yesu ndiye mfano wa mwisho wa unyenyekevu – anatuonyesha jinsi tunavyotakiwa kushirikiana (Wafilipi 2:5).


'Watu wasiolipa baya kwa baya, au laumu kwa laumu, bali wenye kubariki kwa sababu hayo ndiyo mliyoitiwa ili mrithi baraka' (mstari wa 9). Kama Yesu alivyosema, 'Samehe nawe utasamehewa,' Petro anasema, 'Bariki na wewe utabarikiwa.' Kubariki ni kumtakia mwingine mema, na kubadilisha tarajio kuwa maombi. Hivi ndivyo tunavyotakiwa kuwajibu wale ambao sio wazuri kwetu, na inaweza kuwa jambo gumu sana kulifanya.

Kuwatendea wengine hivi husababisha mtindo wa maisha wenye afya, uliobarikiwa na Mungu, hata katika kukabiliana na magumu na mateso.


**LUTENI KANALI JANET ASHCRAFT**

MAREKANI MASHARIKI

Muda wa mapumziko anaoupenda sana Janet ni kuwa na wajukuu wake watatu. Wakati hayuko nao, anafurahia kutembea, kusoma na kucheza michezo. Janet ana shahada ya MA katika Ushauri.

# DUNIA YA MWANAUME

MWANZO 2:18-25

KAPTENI JESSICA WELCH-TURSI

Umewahi kusikia wimbo wa, 'dunia ya mwanaume' uliyoimbwa na James Brown? Ulitolewa mwaka 1966, lakini maneno yake bado yanadumu. Kutoka wakati wa kwanza nilipousikia wimbo huu maneno yake hayajanitoka kichwani. Nimeusikia katika ngozi yangu. Nimeyapitia katika namna nilivyotendewa (au nilivyokosa kutendewa). La kustaajabisha, wimbo unaendelea: 'Lakini ingekuwa si chochote, bila ya mwanamke au msichana.' Naweza kushukuru kwa hizo hisia, lakini bado haionekani kuwa sawa. Nikikua na kuishi katika 'dunia ya mwanaume' imegusa sana jinsi wanawake wanavyojitizama na namna gani waishi sawa na kujitambulisha kwao.

## 'WANAUME NA WANAWAKE WAMEITWA PAMOJA KUMWISHIA NA KUMTUMIKIA MUUMBA WAO.'

Mungu alimuumba mwanadamu kwa mfano wake (Mwanzo 1:26). Mungu wa Utatu bado hajatupoteza. Tunachukua umbo kama udongo mfinyanzi katika mikono yake yenye uwezo. Pumzi yetu ya kwanza inatokana na ya kwake. Pigo letu la moyo la kwanza, ni mwangwi wake. Kwa undani tunathibitisha na mwandishi wa Zaburi: maarifa hayo ni ya ajabu, yanishinda mimi, hayadirikiki, siwezi kuyafikia (Zaburi 139:6). Mwanaume na mwanamke waliumbwa kwa mfano wake. Hapo ndipo tunapopata utambulisho wetu.


'Bwana Mungu alisema: "Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye"' (Mwanzo 2:18). Neno la Kiebrania kuhusu msaidizi ni 'ezer'. Je, Mungu alimuumba mwanamke kuwa msaidizi tu? Mtiifu? Anayepatikana? Je, huo ndiyo utambulisho wetu?

'Ezer' linatumika mara 21 katika Agano la Kale. Katika haya, ni mara mbili tu linaelekezwa kwa mwanamke wa kwanza, Hawa. Mara tatu linaelezea mataifa yenye nguvu ambayo Israeli huwaita waje kusaidia anapozingirwa. Katika nyakati 16 zilizobaki 'ezer' inamwelezea Mungu mwenyewe kama msaada wetu, yeye ajaye na kusafiri nasi wakati wa kutokuwa na msaada (Kutoka 18:4; Kumbukumbu la Torati 33:26; Zaburi 33:20). Hii ndiyo maana ya ***ezer***.

Kama Mungu hayupo chini ya viumbe wake, basi wazo kwamba msaidizi ezer ni duni kwa wengine ni kosa. Agano la Kale halipendekezi 'msaidizi' kama katika 'mtumishi', bali kama mwokozi au mlinzi wetu, kama katika Mungu ambaye ni msaada wetu.' (Zaburi 33:20).

Hapana, hii haitakiwi kuwa 'dunia ya mwanaume'. Ni dunia ya Mungu naye alituumba tukiwa sawa. Bila mwanamke, mwanaume ni nusu ya fumbo. Na, bila shaka, bila mwanaume ni bila mwanamke vile vile.

Kwa kutambua utambulisho wetu wenyewe hakutakiwi kufanya mambo yaegemee moja kwa moja upande tofauti. 1 Wakorintho 13:5 inasema kwamba upendo 'haukosi kuwa na adabu, hautafuti mambo yake, hauoni uchungu, hauhesabu mabaya.'



## JADILI:

* Ni katika njia zipi nimejisikia kuguswa na dhana ya kwamba hii ni 'dunia ya mwanaume? Je, nabeba chuki yoyote au vidonda kwa sababu yake? Chukua muda umkabidhi Mungu yote (kutambua kwamba hii ni hatua, na unaweza kuhitaji kulileta hili mbele za kiti cha enzi tena na tena).
* Itafanana namna gani nikikumbatia utambulisho niliopewa na Mungu wa ezer? Itabadilisha namna gani ninavyojiona mwenyewe? Chaguzi ninazofanya?
* Naweza namna gani kuwawezesha wanawake wengine kukumbatia utambulisho wao kama walio sawa mbele za macho ya Mungu? Hilo linaweza kubadilisha namna gani kikao chetu, jamii yetu, na mji wetu?

Maombi yangu ni kwamba katika kutambua mimi ni nani katika Kristo, sitakosa adabu kwa wengine. Kujiheshimu mimi nilivyo kunatakiwa kunishawishi nisikose adabu kwa wengine. Sitaki kuwa anayetafuta mambo yangu; nataka kuwa anayemtafuta Mungu. Sitaki kukasirishwa na hali ya dunia, nataka nisukumwe nayo na nitafute kuwawezesha wanawake, ezer, kutambua na kukumbatia wao ni nani na wachanue kuwa jinsi walivyoumbwa kuwa.

Kuna hali inayoonyesha kwamba tunauishi utambulisho wetu, kikamilifu na kwa undani, tunapokuwa tuko sawa na bado tuko tofauti, tofauti na bado ni nyongeza, na zaidi ya yote, tunapojifunza kupendana namna hii: kwa kujitoa sadaka kama alivyoonyesha mfano Kristo.

Wanaume na wanawake wameitwa pamoja waishi kwa ajili na kumtumikia Muumba wao. Sasa tunatambua kwamba, kutoka mwanzo, imekuwa ni ujanja wa adui ambaye, anahakikisha wanawake wanabakia wameachwa pembeni, kwa hakika, hudhoofisha uwezo wa wanaume vile vile.

Tunaweza kufikiria tungeweza kupata nini kwa utukufu wake na maendelezo ya ufalme wake kama tungeishi kama watu walio sawa? Kwa hiyo, tunakwenda kufanya nini? Lazima tuchague, kwa pamoja na kwa mtu binafsi, kuishi pamoja, sawa na utambulisho wetu na Mungu na kulingana na muundo wa Muumba wetu, na kwa utukufu wake.

Mpendwa Baba, wewe ndiye mambo yote kwetu. Wewe ndiye Alfa na Omega. Wewe ndiye mwanzo na kusudi letu. Asante kuniumba kwa njia hii ya kufikirika na ya upendo wa namna hii. Nisaidie niukumbatie utambulisho wangu, sio kama msaidizi, lakini kama aliye mtu sawa na wengine katika ufalme wako. Ponya vidonda vya moyo wangu na upande tumaini lenye kina ndani yangu. Niruhusu nione nilitakiwa kuwa nani na ninaweza kuwa nani katika wewe. Amina.

**KAPTENI JESSICA WELCH-TURSI**
ITALIA NA UGIRIKI
Kapteni Jessica anaishi na kutumika Italia pamoja na mumewe, Christopher. Wana wavulana wawili wa muujiza, Liam na Rafaël. Hamu ya Jessica ni kuwakusanya watu mezani, washirikiane kula chakula kizuri, kusikiliza hadithi za watu na kuwaambia habari za Yesu.



# YESU ALITOKA NJE NA AKAGUSA...

MATHAYO 8:1-4

KANALI JULIE FORREST

Mfano wa ujumuishaji mkubwa unapatikana katika Mathayo 8: 'Yesu aliutoa mkono wake nje akamguza mwanaume.'

Ukoma ulionekana kuwa ugonjwa unaoambukiza watu. Kama ulikuwa na ukoma ulitakiwa kuiacha familia yako na mji wako au kijiji chako na uende ukaishi nje – uwe mtu asiye na nyumbani. Wenye ukoma waliwategemea wana familia na marafiki wawaletee chakula na maji wapate kuishi. Kupatikana na ukoma ilikuwa utambuzi mzito. Watu hawakuendelea kupata nafuu kutokana na ukoma; hawakuweza kuwagusa wale ambao waliwapenda kwa hofu ya kuwaambukiza. Kama yeyote alikuwa anawakaribia, walitakiwa kupiga kengele huku wakisema 'asiye msafi, asiye msafi' na wangeishi katika hali hii ya kutengwa hadi kifo.

Tunaweza kufikiria ilivyokuwa kwa mwenye ukoma katika siku za Yesu? Kutengwa na familia na marafiki, mgonjwa, bila kuwa na nyumbani, ukiwategemea wengine kukuletea chakula, kukataliwa na mji wa nyumbani, kupoteza kazi, na mengi zaidi. Nikijifikiria niko katika hali hii, ninaweza kuongeza kwenye orodha hii kupoteza mguso wa kimwili – hii ingekuwa ngumu sana – kukosa kukumbatiwa au kuguswa na mtu mwingine.

Tunaonaje kuhusu mjumuisho? Binafsi, napenda jinsi Yesu anavyoonyesha kuwajumuisha wenye ukoma! Mfululizo wa matukio hapa ni wa maana sana. Kujibu neno la mwenye ukoma, 'ukitaka, waweza kunitakasa' Yesu akanyoosha mkono wake, akamgusa, akisema, nataka takasika'. Richard Beck katika kitabu chake cha Isiyo safi anasema 'Hatua ya kwanza ya Yesu ni kuelekea kwenye unajisi. Kwa kumgusa mwenye ukoma, Yesu kwa makusudi na kwa hiari anatafuta kuambukizwa, akisimama akiwa anawaunga mkono walio wachafu.'

**Ulikuwa mguso wa namna gani wa Yesu kumponya mwenye ukoma? Hili liliendaje nje kuathiri jamii? (tazama kifungu cha 4.)**

Leo tunafahamu mengi zaidi kuhusu ukoma na wenye ukoma hawatengwi tena, hawakataliwi na hawakai peke yao. Alichokifanya hapa Yesu kinazungumza kwa dunia yetu leo kwani watu bado wanajisikia wametengwa. Tunaweza kusherehekea kwamba Yesu alikuja kwa ajili ya wale waliokataliwa na waliotengwa sana.


Somo hili linatualika tufikirie kujumuisha / mweleko wa kijinsia. Mwelekeo wa kijinsia unahusu ni nani tunavutiwa naye kijinsia na kihisia. Kuna mielekeo ya kijinsia mingi, inayojulikana zaidi ni ya jinsia tofauti, mwenye jinsia mbili, shoga na msagaji. Kutokana na mfano wa Yesu, tunatakiwa kuonyesha namna gani kujumuisha wale ambao sio wa jinsia tofauti?

Samuel Wells katika *Tutaishije? (How Then Shall We Live?) Kushiriki Kikristo maswala ya sasa anaandika:* 'Historia ya kutisha, ya mauaji na mateso, ambayo imewaacha wasagaji, mashoga, wa jinsia mbili, )watu waliotengwa sana, walioachwa na waliopungua kanisani inashangaza kwamba bado wapo hapa, watu ambao wanakaribia kipekee kufanana na wale watu waliokuwa karibu na moyo wa Yesu, ushirika na Yesu na huduma ya Yesu.'

Yesu mara nyingi alikuwa rafiki na alifundisha kuhusu wale ambao jamii itawakataa, kahaba, watoza ushuru, wenye ukoma, na akatumia urafiki huu kutufundisha sisi kuhusu kujumuisha.

**Katika Mathayo 21:31 Yesu alisema watoza ushuru na makahaba wanatangulia mbele yenu kuingia katika ufalme wa Mungu – unafikiri ni kwa nini Yesu alisema haya?**

Alipoulizwa kuhusu amri kuu, alitumia mfano wa Msamaria Mwema: 'Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote, na jirani yako kama nafsi yako' (Luka 10:25-37).



## JADILI:

* Jadili hali ilivyo mtu akilazimika kuuficha utambulisho wake halisi wa kijinsia. Kuishi na hofu ya kukataliwa, kuteswa, kubaguliwa na kudhihakiwa kunaweza kuathiri namna gani mtu anavyoishi?
* Utapata changamoto zipi ukionyesha unajumuisha mielekeo yote ya kijinsia katika eneo lako?
* Tunaweza kufanya nini vizuri zaidi?

**Ni nani jirani yako?**

Tunahubiri injili ya 'yeyote', Yohana 3:16, 'Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanae pekee , ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.' Kwanini ni muhimu tufikirie kuhusu kujumuisha watu wenye mielekeo ya kijinsia? Duniani kote wale watu ambao hawana mwelekeo wa kuvutiwa na jinsia tofauti wanalazimika kujifanya ili wakwepe kukataliwa, kuchukiwa, kutengwa, kuonewa na vurugu. Hata ndani ya kanisa wanajisikia hawawezi kujidhihirisha walivyo kwa hofu ya kuhukumiwa. Maoni na mienendo ya chuki huumiza na kuharibu na inaweza kusababisha watu wafikirie kujidhuru au kujiua. Je, Yesu angewapita au angewafikia na kuwagusa? Angewapa upendo wa Mungu usio na masharti, akiwaacha wafahamu kwamba kupitia kwa mateso yake na kifo chake alifanya upatanisho kwa ajili ya dunia yote? Kwamba hata wao hawahitaji kuangamia, lakini wanaweza kuupata uzima wa milele, kwamba hata wao sio wabaya, wao pia ni watoto wa Mungu?

## 'KWA KUMGUSA MWENYE UKOMA, YESU KWA MAKUSUDI NA KWA HIARI ANATAFUTA KUAMBUKIZWA, AKISIMAMA AKIWA ANAWAUNGA MKONO WALIO WACHAFU.'

Tunatakiwa kuwatendea watu namna gani? Napata jibu katika Wakolosai 3:12-14: 'Basi kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake, kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi. Zaidi ya hayo yoye jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu'.

Naomba Roho Mtakatifu wa Mungu atupe changamoto sisi kila mmoja tuchukue hatua, hata hatua ndogo, kuelekea kwenye kujumuisha.

Bwana nisaidie nionyeshe upendo na huruma yako kwa watu wote ninaokutana nao, naomba hata mimi pia niguse maisha ya wengine kwa mjumuisho. Amina

**KANALI JULIE FORREST**
MAKAO MAKUU YA KIMATAIFA
Kanali Julie Forrest anatumika Makao Makuu ya Kimataifa kama Afisa wa uhusiano anayehusika na Mazungumzo kuhusu Ujinsia wa Binadamu. Julie ameolewa na Petro kwa miaka 35 na wana wavulana wawili na wajukuu wawili. Moyo wa Julie ni kwa watu na haki ya jamii.



# UPENDO AMBAO UNAFIKIA VIZAZI

RUTHU 1:1-22

MEJA LEANNE BROWSKI

## 'UHUSIANO KATI YA RUTHU NA NAOMI UNAONYESHA KUTEGEMEANA KUZURI KULIKO NA MANUFAA YA PANDE ZOTE KUNAKOSAMBAA VIZAZI VIWILI TOFAUTI NA TAMADUNI MBILI TOFAUTI.'


Ukisema neno 'mama mkwe' mara nyingi unapata majibu ya tofauti, hasa kutoka kwa wanawake ambao wamepitia mahusiano na mama wakwe. Wengine wanaweza kutabasamu, na kuelezea kushukuru kwa upendo, ushauri na kukubalika walikopokea kutoka kwa mama mkwe, wakati wengine watapindua macho yao, na kupumua kwa nguvu na kuzungumza kwa kina kuhusu uvumilivu wakati wao wa mahusiano ya changamoto na mama wa mume wake mpendwa. Sijui kama Ruthu alipata ya sehemu zote mbili za shilingi katika mahusiano yake na Naomi?

Njaa ilipoikumba Bethlehemu (maana yake 'nyumba ya mkate') tunaona kwamba Elimeleki alimchukua mkewe Naomi, na wavulana wake wawili Maloni and Kilioni, hadi Moabu ambako ardhi ilikuwa na rutuba, na chakula kilikuwa kingi. Kutokana na historia kati ya Israeli na Wamoabu kuhama huku kulikuwa muhimu na hata zaidi yale maendeleo yaliyofuatia (hesabu 25). Wakiwa wanaishi Moabu, Maloni na Kilioni walioa akina mama na majina yao ni Orpa na Ruthu. Wageni katika nchi ya kigeni, Elimeleki na familia yake wakaanza kutengeneza maisha yao bila shaka wakitumaini siku njema zinakuja. Kwa huzuni, haikuwa hivyo kwani Elimeleki alifariki na miaka 10 baadaye wote Maloni na Kilioni walifuata. Naomi sasa ni mjane anayeishi katika nchi ya ugenini, watoto wake wote wamefariki. Kuwa mjane ilionekana kuwa ni jambo zito lakini kuwa mjane halafu huna mtoto ilionekana kuwa ni laana, na hivyo kilichoonekana hapo nyuma kuwa na siku zijazo zilizo njema kwa wanawake wote watatu mara zikawa ni giza.

Aliposikia kwamba hali ya chakula Bethlehemu inaendelea kuwa nzuri na kwa kuwa hakuwa na sababu ya kuendelea kuishi Moabu, Naomi aliamua kurudi nyumbani. Wote Orpa na Ruthu wako tayari kwenda naye Naomi, lakini anawasisitizia kwamba itakuwa vizuri wakibaki. Orpa shingo upande alichagua kubaki, Ruthu alifanya uamuzi wa kwenda. Sio Orpa wala Ruthu alikosa kumheshimu Naomi kwa uchaguzi wake, lakini Ruthu alienda hatua moja mbele ya Orpa. Ruthu alipenda zaidi na akataka kumheshimu Naomi kwa kuweka masilahi ya mama mkwe mbele ya yale ya kwake. '[Upendo] haukosi kuwa na adabu, hautafuti mambo yake, hauoni uchungu, hauhesabu mabaya' (1 Wakorintho 13:5). Ruthu angeweza kubakia mahali alipopazoea, ndani ya nchi yake, katika utamaduni wake, mahali alipokuwa na ndugu, akiabudu miungu yao, pakiwa na matarajio ya kuolewa tena. Kwa kweli, hilo lilikuwa jambo la 'busara' kufanya! Lakini Ruthu hafanyi hivyo. Ruthu anaonyesha upendo mkubwa kwa Naomi.

Neno la Kiebrania kwa aina hii ya upendo wa kujitoa sadaka ni 'Hesed'. Hesed limezama katika ibada, likionyesha kuhusika kwa dhati kwa mtu mwingine na ni ushahidi kupitia kwa matendo. Jibu la Ruthu kwa msisitizo wa mama mkwe wake kwamba abaki Moabu kunaonyesha hali yake ya ibada ya moyo na kujitoa kisadaka kwake Naomi: 'Usinisihi nikuache, nirejee nisifuatane nawe; maana wewe uendako nitakwenda, na wewe ukaapo nitakaa. Watu wako watakuwa watu wangu, na Mungu wako atakuwa Mungu wangu' (Ruthu 1: 16).

Uhusiano kati ya Ruthu na Naomi unaonyesha kutegemeana kuzuri kwa pamoja kuliko na faida kunakosambaa vizazi viwili tofauti na tamaduni mbili tofauti. Tunaona jinsi utii wa Ruthu, kujitoa kwake na mwingiliano na



## JADILI:

* Una uhusiano wa namna gani hivi sasa na wale ambao ni wakubwa na wale ambao ni wadogo kwako?
* Unawezaje kuonyesha huu upendo wa 'hesed' kwa wale ambao ni wakubwa na wadogo kwako?
* Unaweza kutumia namna gani ugumu ulio nao hivi sasa kukisaidia kizazi kinacho kufuata?

Naomi unafungua dunia mpya kwa mama mkwe aliye na majonzi. Naomi, anayejieleza kuwa ni 'mchungu' (Ruthu 1:20) na 'hana kitu' (Ruthu 1:21) na anakabiliana na dunia akiwa na mtazamo wa kukata tamaa unaotokana na kuvunjika kwake na kupoteza, akaja kupata tumaini jipya, familia mpya na siku nzuri zijazo. Naomi aliyejiona hana cha kumpa Ruthu, akampa zaidi kwa kumwongoza na kumshauri Ruthu jinsi ya kupita katika utaratibu ambao ulikuwa mgeni sana kwake (Ruthu 3:1-4). Hii ilimwongoza Ruthu kwa mume wake mpya, maisha mapya, kwa mtoto wa kiume na akapata nafasi katika ukoo wa Yesu Kristo. Ruthu, mjane asiye na mtoto, mkimbizi katika nchi ya kigeni anapata heshima, anakubalika na anapata daraja jipya wakati wanawake wa Israeli walitangaza kwa Naomi kwamba upendo ambao Ruthu amemwonyesha ni zaidi ya baraka ya kuwa na watoto wavulana saba (Ruthu 4:14-15). Sifa ilikuwa hasa kutoka wakati wa historia ambao watoto wa kiume walionekana kuwa chanzo cha usalama, kuhudumiwa, ulinzi na baraka ya Mungu.

Naomi yuko tayari kumfundisha Ruthu mambo asiyoyajua (Ruthu 2:22; 3:1-4). Kila kizazi kabla ya chetu kina hekima, uzoefu na uwezo wa kutusaidia tupite katika barabara tuliyomo. Uelewa wa maisha wa Naomi, utamaduni na siasa za familia vilimsaidia Ruthu aipate njia katikati ya njia zisizojulikana. Ruthu alikuwa wa kufundishika na alikuwa tayari kujifunza kutoka kwa mama mke wake (Ruthu 3:5) kilichosababisha akamate usikivu na hatimaye moyo wa Boazi (Ruthu 4:9-10).

Maumivu makali ya Naomi katika sura ya mwanzo ya kitabu cha Ruthu yanageuzwa na pazia linapofungwa kuhusu hadithi ya Ruthu, tunaona kwamba kupitia kwa Boazi na Obedi, Naomi anapata urithi na siku zijazo ambazo alidhani hazitakuwa zake. Kumbukumbu la Torati 25:5-6 inaonyesha kwamba mtoto wa thamani wa kiume huyu anabeba jina la ukoo wa Elimeleki. Tunaona kupitia kwa Naomi, Ruthu anapata kukubalika, heshima ya wengine, anapata mume na mahali katika jina la familia linaloendelea kusikika katika nyakati. Vizazi viwili, wakipendana na kujifunza pamoja, wakijifunza na kuokota masazo mmoja kwa mwingine, kila mmoja akimhitaji mwenzie, wakitembea kupita katika maji ya kina. Hata hivyo, jambo moja kubwa lilikuwa likijifunua kupitia kwa hadithi yao. Naomi na Ruth wasingeweza kufahamu kwamba matukio haya, ingawa kuna giza, hofu na kukata tamaa wakati fulani, vyote vilikuwa sehemu ya Mungu kumwinua mfalme wa Israeli atakayekuja kunyonga majitu, atawaongoza watu wake kwenye ushindi mwingi mkubwa, na zaidi ya yote, atakuwa mtu wa moyo wake mwenyewe. 'Bali fadhili za Bwana zina wamchao tangu milele hata milele, na haki yake ina wana wa wana' (Zaburi 103:17).



Mpendwa Bwana, naomba upendo wangu kwa vizazi vilivyoko mbele yangu na vizazi vitavyonifuata mimi viwe kama vile vya Ruth na Naomi, na naomba wewe utukuzwe kupitia katika vyote.

**MEJA LEANNE BROWSKI**
AFRIKA YA KUSINI
Leanne anatumika pamoja na mume wake kama viongozi wa sehemu huko sehemu ya Kwa Zulu Natal ya Kati. Leanne ameolewa na Brendan kwa miaka 24, amekuwa afisa kwa miaka 19 na anashukuru kuwa mama wa vijana watatu wa ajabu. Kumpenda Yesu na kuwapenda wengine kunamletea Leanne furaha kubwa na anajitahidi aweze kufanya vyote kwa uhalisia na kwa ubunifu.



# KUWAJUMUISHA NA KUWAHESHIMU WENGINE KATIKA KUTAFUTA USAWA WA KIJINSIA

YOHANA 4:4-26

MEJA MARGARET STAFFORD

Yesu alipoulizwa na msomi wa sheria: 'ni amri ipi iliyo kuu?' (Mathayo 22:36), Yesu hata hakuwa na haja ya kufikiri. Alimrudishia mtu huyo ile sheria. Wayahudi wanaume kwa wanawake walijifunza sheria toka utotoni – mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote. Lakini Yesu aliongezea ya pili, ambayo nayo ina uzito ule ule nayo ni 'mpende jirani yako kama nafsi yako' (Mathayo 22:39). Sehemu hii ya sheria haijazingatiwa kama ile sehemu ya mwanzo.

Nilipata hili kwenye mtandao wa Vito vya Kiyahudi:

'Kumpenda Mungu, hata hivyo, hakuhesabiwi kuwa ni mfano sahihi wa maisha ya Kiyahudi. Hata muhimu zaidi, kama ilivyoelezwa katika kanuni ya maadili ya Kiyahudi toleo la 1 (*A Code of Jewish Ethics Volume 1)* na Rabi Joseph Telushkin, ni upendo wa jirani. Kwa nini? Kwa sababu upendo wa mtu kwa jirani yake unakuwa ni kipimo cha mtu huyo kwa Mungu. Nini ni muhimu zaidi kwa Mungu? Kulingana na Rabi Akiva (*Jerusalem Talmud*, Nedarim 9:4), "Mpende jirani yako kama nafsi yako; hii ndiyo kanuni kuu ya Torati." Katika akili za Wayahudi, kuna fumbo kila upande wa alama zinazofanana. Mpende Mungu = mpende jirani yako.'[1]

Naamini msomi wa Kiyahudi alikuwa anatambua haya. Lazima alitambua kwamba huwezi kumpenda Mungu kama haumpendi jirani yako. Unaweza kujiuliza hili limeendaje kwenye usawa, haki hata na maisha kama tunavyoyaishi leo. Jibu langu: kila kitu!

Kwangu mimi, usawa ni jambo ambalo hatuwezi kulikamata kwa kweli. Tunaishi katika jamii isiyo na usawa, ndiyo maana tuna mapambano haya dhidi ya haki ya jamii na ni sababu ya kwa nini tupo kama shirika la hisani na kama kanisa. Maisha hayako sawa. Wengine wanazaliwa ikulu, wengine wanazaliwa mazizini. Lakini hatuangalii usawa (equality) (*kila mmoja anapewa rasilimali au nafasi sawa bila kujali tofauti zao*), tunaangalia usawa (equity) (*kwa kutambua tunatofautiana hivyo tunapata rasilimali na nafasi zinazohitajika kutuwezesha kufikia mwisho ulio sawa)*.

**'USAWA WA KIJINSIA UNATAMBUA KWAMBA KILA MMOJA WETU NI WA MUHIMU KWAKE MUNGU.'**


Tazama Zaburi 99:4 inazungumza kuhusu Mungu anayekaa kwenye mamlaka kati ya Makerubi: 'Nguvu za mfalme nazo zapenda hukumu, wewe ndiwe uliyeithibitisha adili, ulifanya hukumu na haki katika Yakobo.'.

Mfano mwingine, kuzungumza juu ya Daudi katika 2 Samweli 8:15: 'Daudi akatawala juu ya Israeli wote, naye Daudi akawafanyia hukumu na haki watu wake wote.'

Neno la Kiebrania la usawa ni (mê-šā-rîm) linaweza kuwa na maana ya unyoofu, kunyooka, tambarare, haki, kweli, utaratibu na maadili. Katika Kitabu cha ufafanuzi cha Biblia ya Kiwango cha Kimataifa, (International Standard Bible Encyclopaedia), usawa unaelezwa kuwa ni 'roho ya sheria iliyo nyuma ya barua; haki ni utekelezaji wa roho ya usawa'.[2]

Mwanaume aliumbwa na Mungu kutoka katika mavumbi na akatambulishwa kwenye ulimwengu wa viumbe vinavyoishi na mwanamke aliumbwa na Mungu kutoka kwenye mfupa. Kutolewa kutoka kwa mwanaume, na kumtambulisha kwa mwanaume, Mungu anatoa tangazo la ulinzi: 'Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja.' (Mwanzo 2:24). Yesu anaongezea, 'Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe' (Mathayo 19:6).

1 (https://www.jewishjewels.org/blog/love-god-love-your-neighbor)
2 What Does the Bible Say About Equity vs. Equality – The Religion and Politics Blog (nealhardin.com)



## JADILI:

* Nabeba matendo, mienendo na mawazo gani katika moyo wangu ninapozungumza na kila mmoja ambaye hafanani na mimi?
* Kumfahamu Yesu kunabadilisha namna gani matendo, mienendo na mawazo yangu?
* Nawezaje kutoa nafasi na kujenga matarajio kuhusu watu binafsi, bila kujali jinsia?

Kwa kweli tunahitajiana. Mungu mwenyewe alisema sio vema kwa mwanaume kuwa peke yake nami naamini kwamba sio vizuri vile vile kwa mwanamke kuwa peke yake.

Tunapoteza mwelekeo wa kusudi lenyewe la uumbaji wetu – kuujali uumbaji wa Mungu, na kufuatana na Isaya sisi ni 'watu wale niliojiumbia nafsi yangu, ili wazitangaze sifa zangu' (Isaya 43:21). Tuliumbwa kimakusudi kwa kusudi. Sio tupigane mmoja na mwingine bali tukamilishane mmoja na mwingine.

Kumpenda jirani kunaelezwa namna gani katika usawa wa jinsia? Hebu tutizame tofauti za haya mawili: 'Usawa wa kijinsia ni matendo, mienendo na mawazo yanayotoa nafasi na kujenga matarajio kuhusu watu binafsi bila kujali jinsia.[3]

Maelezo mengine ni: 'Usawa (equality) huzingatia kujenga mstari mmoja wa kuanzia kwa wote. Usawa (equity) unalengo la kumpa kila mmoja viwango vyote vya nafasi na faida – mwisho mmoja ulio sawa.'[4]

Usawa wa jinsia unatambua kwamba kila mmoja wetu ni wa muhimu kwa Mungu na kwamba Mungu hutuangalia kama kilele cha uumbaji wake, hakuna zaidi – lakini bila shaka hapana pungufu. Sisi sote ni watafutaji, wote wanaume na wanawake, tunatafuta moyo wa Mungu, tunatafuta mapenzi yake kwa maisha yetu na tunatafuta mapenzi yake kwa wale tunaowapenda.

Mfano maridadi wa usawa wa jinsia katika matendo ni ule wa katika hadithi ya mwanamke kisimani. Kuwa ya haki katika maisha ya mwanamke huyu. Alifahamu nini maana ya kupendwa na kuachwa, kuepukwa na wanawake katika mji. Alifahamu nini maana ya kulelewa kama Msamaria – 'nusu mzawa' kuepukwa na jamii ya Kiyahudi kwa sababu ya mchanganyiko wa damu yake.

Ndiyo Yesu anamtafuta na anamwomba maji. Soma hadithi yake katika Yohana 4:4-26. Jambo moja linalomgusa mwanamke huyu kuhusu huyu mwanaume ni utambuzi wake usio wa hukumu – jambo ambalo hakulitarajia kwa wote waliomfahamu. Alifahamu kwamba Yesu alifahamu yote juu yake na bado alimpa maji wa uzima.

---

3 Women's Educational Equity Act (Equity Resource Centre)
4 https://www.ywcalgary.ca/news/equity-v-s-equality-whats-difference/

Mungu atusaidie tuupende uumbaji wake kama yeye anavyoupenda. Baba, tufundishe tujue kwa kweli ina maana gani kumpenda jirani kama tunavyojipenda wenyewe. Kwa kufanya hivyo tutakudhihirisha wewe kwa uwazi zaidi katika yote tunayoyafanya. Amina.

**MEJA MARGARET STAFFORD**
MASHARIKI YA KATI
Mimi ni binti ya wazazi maafisa, mke wa Jeff na mama ya Natalie, Nicole, Matthew na Mark na, muhimu zaidi, bibi yake na Kaylie, Benjamin na Daniel, Nikoli, Keanu na Connor. Kwa sasa nafanya kazi kama sehemu ya timu ya uongozi ya Mashariki ya kati. Naishi Umoja wa Falme za Kiarabu nikiishi Abu Dhabi. Na hesabu kwamba ni upendeleo mkubwa kufanya kazi katika chungu hiki kinachoyeyuka cha mataifa, utamaduni na imani.



# MALI YA

WAGALATIA 3:28

MEJA MARIE DAVIS

'Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu.' (Wagalatia 3:28).

Kufuatana na kamusi ya Merriam-Webster neno 'mali ya' lina maana 'kustahili, kuwa sahihi, au kuwa na upendeleo; kuwa mali ya mtu au kitu cha mtu'.

Hakuna anayependa kujisikia mpweke, kutokupendwa na hajaungana na wengine. Mungu alituumba tuwe wa mahusiano kitu kinachotufanya tujisikie tumeshukuriwa na tu sehemu ya kitu kikubwa. Halikuwa kusudi la Mungu sisi tuwe peke yetu bila ya familia au marafiki. Alilionyesha hili katika Mwanzo 2:18: 'Bwana Mungu akasema, "Si vema huyu mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye."'

Mungu alimuumba mwanadamu na akatoa nafasi ya sisi kufurahia ushirika na wengine. Hapa kuna vipengele muhimu vya kufikiria kama watoto wa Mungu tunapo tafakari juu ya nini maana ya kuwa mali ya: Wewe haujatengwa – wewe ni mali ya:

'Jueni kwamba Bwana ndiye Mungu, ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake; tu watu wake na kondoo wa malisho yake.' (Zaburi 100:3).

Hii inathibitisha kwamba sisi ni mali ya Mungu. Sisi ni mali yake, hatujatengwa na Mungu badala yake, 'Ni yeye aliyetutengeneza, na sisi ni wake.'

Mazingira katika maisha yanaweza kutufanya tupooze na kutufikisha mahali tunajisikia tumeachwa, sisi sio sehemu yake na tumesahauliwa. Kukabiliana na changamoto za maisha haiwezi kuepukika. Hata hivyo, changamoto zetu haziwezi kubadilisha pale ambapo sisi ni mali yake. Tunabakia kuwa 'watu wa Mungu na kondoo wa malisho yake'.

'Nchi na vyote viijazavyo ni mali ya Bwana, dunia na wote wakaao ndani yake (Zaburi 24:1).

Mwandishi wa Zaburi anatupa mwelekeo, kusudi na ukamilisho. Hayupo hata mmoja ambaye ametengwa, wewe na mimi ni sehemu ya 'wote wanaoishi ndani yake' hii maana yake sisi sio yatima wala waliotupwa mbali.

Aliyoyatoa kwetu Mungu husababisha tuwe mali yake kwa kweli. Kuwa mali yake kikweli ni kujulikana kikamilifu na kupendwa kikamilifu.

Kuishi tukikataa kukubali sisi ni nani na sisi ni mali ya nani kunaweza kugusa maisha yetu vibaya na ikajifunua kama kuto kujithamini ipasavyo, bila tumaini, wenye hofu na kukataliwa. Hata hivyo, kuelewa thamani yetu na sisi ni mali ya nani huturuhusu tuyashughulikie yale yetu yaliyo kinyume, jambo ambalo hutuweka tuwe imara kiakili katika maisha yetu ya kila siku. Tunaweza kupata hakikisho hili katika Maandiko: 'Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi..' (Yeremia 29:11); 'Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, (Waefeso 2:10).

Maandiko mengine huthibitisha wapi na ni nani ambaye sisi ni mali yake na kutukumbusha kwamba sisi tuliumbwa na Baba yetu wa mbinguni. Yeye huhakikisha anatutunza, akituhakikishia kupitia kwa neno lake kwamba sisi hatuko peke yetu na kwamba sisi ni wa kwake.

Manufaa ya kuwa mali yake ni yapi?

'na kama tu watoto tuwarithi, warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo, maana tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye' (Warumi 8: 17).

## (A) WARITHI

Mrithi anaweza kuelezwa kuwa ni mtu anayepokea sehemu ya mali iliyo yake kwa sababu ya haki ya kuwa mwana.



**JADILI:**

* Unajisiki kwamba wewe ni sehemu ya kile ambacho Mungu amekupa?
* Unaelewa jinsi ulivyo wa thamani kwa Mungu?
* Uko tayari kufanya nini, kuhakikisha unafurahia faida ambazo Mungu kakuwekea?

Kulingana na kitabu cha ufafanuzi cha *Matthew Henry*, 'Katika urithi wa duniani sheria hii haina mshiko, ni watoto wa kwanza tu ndiyo warithi; lakini kanisa ni kanisa la wazaliwa wa kwanza, kwa sababu wote ni warithi. Mbinguni ndiyo urithi wa watakatifu wote.'

## 'MUNGU ALIMUUMBA MWANADAMU NA AKATOA NAFASI YA SISI KUFURAHIA USHIRIKA NA WENGINE.'

Biblia ilitoa ufafanuzi katika Mwanzo 25:29-34 wa Esau ambaye kwa haki ndiye aliyetakiwa kupokea haki ya mzaliwa wa kwanza kama mzaliwa wa kwanza. Hata hivyo, hakuthamini kabisa nafasi yake ya upendeleo akaiuza kwa Yakobo mdogo wake, ambaye sawa na sheria hakutakiwa kushiriki katika urithi huu.

Kama warithi wenza na Kristo hayupo mtoto wa kwanza wala wa mwisho, wote sisi tuko sawa na tunashirikiana katika upendeleo na faida iliyo sawa.

### (B) USALAMA

'Kwa kuwa Bwana atakuwa tumaini lako, naye atakulinda mguu wako usinaswe' (Mithali 3:26).

Kondoo walioachwa peupe watakuwa katika mazingira hatarishi kushambuliwa na mbweha lakini akiwepo mchungaji analinda watakuwa salama. Sisi sote hujisikia tupo katika mazingira hatarishi ya mambo ya uovu yanayotuzunguka; kutokuwa na uhakika wa maisha wakati fulani hutuweka katika mazingira ya hofu. Mchungaji na mwandishi Rick Warren alisema: 'Usalama wa kweli unaweza kupatikana tu katika kile ambacho hakiwezi kuchukuliwa kutoka kwako – mahusiano yako na Mungu.' Usalama ni moja ya faida kubwa tunazopata kama watoto wa Mungu. Hata hivyo, hii haina maana kwamba tumesamehewa kushambuliwa. Ina maanisha tu kwamba tuna ujasiri wa kuondoa hofu yetu na kwamba hatukabiliani na maadui zetu peke yetu.


Baba yetu wa mbinguni hutupa ushindi sisi watoto wake, kwa hiyo hutupa kujumuika. Yeye sio sehemu, mchaguzi wala haonyeshi upendeleo, badala yake yeye ni wa haki, na usawa.

Faida nyingine za kufikiria:

- Mawasiliano ya wazi: 'Nanyi mtaniita, mtakwenda na kuniomba, nami nitawasikiliza' (Yeremia 29:12).
- Mtoaji wa vitu: 'Na nani anayempatia kunguru chakula, makinda wake wanapomlilia Mungu, na kutanga tanga kwa kutindikiwa na chakula?' (Ayubu 38: 41).
- Nidhamu: 'Basi mkiwa kama hamna kurudiwa, ambako ni fungu la wote, ndipo mmekuwa wana wa haramu, wala si wana wa halali' (Waebrania 12:8).

Mpendwa Baba, tupe hekima ya kukubali ahadi na uhakikisho uliotupa kupitia kwa neno lako, kwamba sisi ni mali yako, na wewe unatupenda hadi milele. Amina.


**MEJA MARIE DAVIS**
CARIBBEAN

Nilizaliwa Jamaica, na pamoja na mume wangu Meja Desmond Davis, tumekuwa maafisa wa Jeshi la Wokovu kwa miaka 22 na pamoja sisi ni wazazi wa watoto wetu wawili, Abigail na Jeremy. Sisi ni maafisa wa vikao vya Havendale na Kintyre huko Jamaica Mashariki,na nashikilia wadhifa mwengine wa ziada wa Katibu wa Sehemu wa Huduma ya Wanawake. Nafurahia kupata marafiki wapya na kuangalia mchezo maarufu uwanjani.

# UWANJA WA HURUMA: FUNDISHO KUTOKA KWA RUTHU

RUTHU 1:16

KAPTENI MARTA GOVERNO

‘Naye Ruthu akasema, usinisihi nikuache, nirejee nisifuatane nawe; maana wewe uendako nitakwenda, na wewe ukaapo nitakaa. Watu wako watakuwa watu wangu, na Mungu wako atakuwa Mungu wangu"' (Ruthu 1:16).

## UTANGULIZI

Ruthu ndicho kitabu ninachokipenda katika Biblia. Nimekisoma na kuhubiri kwa kukitumia mara nyingi na lazima nikubali kwamba kila ninapofanya hivyo najifunza jambo jipya! Nakipenda kitabu hiki kwa sababu nafikiri kina toa taswira ya mengi ambayo Yesu (na Agano Jipya kwa ujumla) wametufundisha kuhusu kuwajali wengine. Kwa hiyo, kuwafikiria watu wenye ulemavu, tunaweza kujifunza nini kutoka kwa Ruthu na wale wengine?

## 1) KUWA TAYARI KUBADILIKA/KUJIFUNZA (SURA YA 1)

Naomi ameachwa mjane na bila mtoto katika sehemu ya kigeni. Ingawa yeye sio ‘mlemavu’, lazima tukumbuke kwamba, wakati wake, hali yake ingemfanya awe katika mazingira magumu sana. Kwa hiyo aliamua kurudi nchini kwao Bethlehemu, ingawa hata huko atakuwa bado katika mazingira magumu. Wake za watoto wake wangeweza kirahisi kubakia na familia zao, lakini Ruthu alichagua kwenda pamoja na mama mkwe wake.

**‘NI MUHIMU KWAMBA TUKO RADHI KUJIFUNZA ZAIDI KUHUSU DUNIA YAO NA TUBADILISHE NJIA ZETU ILI TUWEZE KUWASAIDIA VIZURI ZAIDI.’**

Katika tendo hili ndipo palipo na fundisho letu la kwanza: Utayari wa Ruthu kubadilika/kujifunza. Wakati wa kuwafikiria watu, hasa wale wenye ulemavu, ni muhimu tuwe radhi kujifunza zaidi kuhusu dunia yao na tubadilishe njia zetu ili tuweze kuwasaidia vizuri zaidi! Tunaelewa kwa kweli ilivyo vigumu kwa mtu kwenye kiti cha magurudumu kuingia katika jengo lisilokuwa na njia za kupitia? Au kwa wazee wanaotumia mikongojo kupanda basi.

Kwa njia hiyo hiyo Yesu alikuja duniani kwetu aishi tunavyoishi. Wakati mwingine tunatakiwa tutoke katika sehemu zetu, kama Ruthu alivyofanya.

## 2) KUJALI KULIKO ZAIDI YA WAJIBU (SURA YA 2)

Sheria ya Israeli inayowahusu watu walio katika mazingira magumu katika jamii yao. Sheria nyingi ziliwalinda (yatima, wajane, maskini...). Hakuna kilichokuwa cha ajabu kuhusu kuchukua hatua za makusudi kusaidia hili kundi katika umma. Kwa mfano, wakati wa mavuno, wafanyakazi hawakuwa wanakusanya mabaki ya mazao ili maskini waje nyuma yao na waokote masazo.

Hili ndilo analofanya Ruthu kwa ajili yake na Naomi wapate chakula, na wakati huu anakutana na mtu mwingine ambaye atatupa fundisho: Boazi. Shamba ni mali yake na, kama Mwisraeli yeyote mwema, huwaacha watu waokote masazo ya nafaka. Hata hivyo, anakwenda zaidi ya wajibu wake wa kawaida na akamwambia msimamizi wake ampe Ruthu nafaka ya ziada, akawa anaacha nafaka nyingi zaidi nyuma kwa ajili ya Ruthu.



## JADILI:

* Unafahamu kiasi gani cha changamoto ambazo walemavu wanakabiliana nazo katika jamii yako? Unaweza kuzifahamu vizuri zaidi namna gani?
* Ukiwa niani unakumbuka tulichojifunza kuhusu kitabu cha Ruthu na vifungu vya msaada, sisi kama Wakristo tunawezaje, kuonyesha mfano wa kuwajali watu wenye ulemavu?
* Tunawezaje kuwapa nafasi watu wenye ulemavu watumike?

Mara nyingi sisi hujisikia tunafanya ya 'kutosha' kwa ajili ya wenye ulemavu katika jamii yetu. Huenda tunatoa msaada wa fedha kwa vikundi vya hisani au tunajitolea kwenye matukio yao. Lakini tuko tayari kwenda zaidi ya hapo? Itafananaje sisi kama Boazi, kama tutakwenda umbali wa ziada kuhakikisha watu wanapata kile wanachohitaji? Ruthu na Naomi walikuwa wanawake wawili wajane katika jamii wasio na nafasi, kama wenye ulemavu wengi katika jamii leo.

### 3) KULIPA GHARAMA (SURA YA 3 NA 4)

Mara tena kwa kutumia sheria, Naomi anatambua kwamba Boazi anaweza kuwasaidia zaidi kwa kukomboa mali yao na kumuoa Ruthu. Boazi alipotambua kuhusu uwezekano huu, alihakikisha hatua zote zinazostahili zinafuatwa, akamwahidi Ruthu atashughulikia swala hili. Kwake Boazi, maneno ni kujitoa: siku ile ile aliyomwambia Ruthu, alitekeleza. Alipomuoa Ruthu, walimlea Naomi na wakapata mtoto.

Boazi hakuwa tu 'anazungumza' kwani alikuwa tayari kulipa gharama ili awasaidie Ruthu na Naomi, sio kwa nafaka tu bali kwa kuyabadilisha maisha yake mwenyewe kuhakikisha wana msaada wanaohitaji. Kuwasaidia watu sio tu kuhusu kuwapa vitu (fedha, chakula, n.k.), ni kutambua nini kingine tunaweza kufanya kubadilisha hali zao. Watu wenye ulemavu wanaweza wasiweze kubadilishiwa mapungufu yao, lakini wanaweza kubadilishiwa mazingira yao! Maneno yetu yanatakiwa kuwa ni kujitoa vile vile. Wakati fulani tunatakiwa kuachana na maeneo yetu ya starehe ili tuweze kubeba mahitaji ya wale wanaotuzunguka.

**Vifungu vinavyounga mkono:** Wafilipi 2:3-4; Wagalatia 6:2.

Mpendwa Bwana, wakati fulani tuna hatia ya kuishi maisha yetu ya kutengwa na mahitaji ya watu wenye ulemavu katika jamii zetu. Tafadhali tupe mioyo iliyo tayari kujifunza, kujali zaidi ya wajibu, na tuwe tayari kulipa gharama. Amina.

### KAPTENI MARTA GOVERNO

UHISPANIA NA URENO

Kapteni Marta ni Mreno naye anatumika kama afisa wa Jeshi la Wokovu katika teritori ya Uhispania na Ureno ambako, wakati wa kuandika haya, alikuwa mkurugenzi wa Kituo cha Malezi ya watu Wazima huko Porto. Ameolewa na ana binti wa miaka saba. Kufundisha ni moja ya maeneo anayoyapenda katika huduma. Anapohitaji kujiongeza na kwenda sambamba tena na Mungu hupenda kuwa karibu na bahari, kwa hiyo likizo za baharini ndizo anazozipenda zaidi.



# TAIFA NA UTAMADUNI – UTOFAUTI: NJIA YA UTUKUFU NA HESHIMA YA MUNGU

## WARUMI 15:7

MEBLE VILIKA BIRENGO

'Kwa hiyo mkaribishane ninyi kwa ninyi, kama naye Kristo alivyotukaribisha, ili Mungu atukuzwe.' (Warumi 15:7).

Haipo nafasi bora zaidi ya kuzisikia changamoto za utofauti katika utamaduni na utaifa kuliko kukua kama mtoto wa maafisa wa Jeshi la Wokovu. Nakumbuka kufunga na kufungua mizigo kila miaka mitatu wakati wazazi wangu walipopokea uhamisho, na kulazimishwa kurithi, kuungana na kusonga mbele haraka iwezekanavyo. Hata hivyo, hii haikuwa sehemu yenye changamoto kubwa katika uhamisho. Changamoto ilikuwa kujikuta niko katika utamaduni nisiouzoea wenye matarajio ya jamii na kuhangaika kupata uwiano ulio sawa kati ya kuwa mdogo na hamu ya kuwa huru kufanya yale ambayo yalikuwa ya kawaida kwangu, wakati nikiishi katika utamaduni usio wa kawaida.

**'KAMA WATU WA MUNGU LAZIMA TUOMBE MACHO YETU YA KIROHO YAFUNGULIWE TUYAONE MAISHA KWA JICHO LA MUNGU.'**

Kama mtu mzima, nimepitia kiwango hiki cha utofauti katika matukio mbalimbali. Niliishi Bangladeshi kwa miezi miwili kwenye mpaka na India, nikishauri timu ya vijana tulipokuwa tukishawishi majibu ya maendeleo ya jamii. Kama mwanamke kijana mweusi, mwenye nywele ndefu zilizosokotwa na mwenye lafudhi ya Kenya, kwa dhahiri 'nilionekana' katika macho ya jamii. Nakumbuka kutembea kwenda kutembelea familia na watoto wakipanda mitini wapate japo kidogo kuniona. Wengi wao hawajapata kumwona Mwafrika kabla na makundi yalinifuata kila mahali nilipo kwenda. Hii inaweza kufanana na hadithi tunayoisoma katika vitabu, lakini ukweli na uwezo katika wakati huo katika mahusiano sawa na mada ya wengine, utaifa na utamaduni ni mambo muhimu sana.

Kama Wakristo, tunatakiwa kutambua kusudi la Mungu kwa watu wake ambao sisi tunawaona kuwa wa tofauti. Tunatakiwa kuthamini thamani ya tofauti zetu kama Mungu anavyoagiza. Warumi 15:7 ni ukumbusho wa msingi wa kumpokea kila mmoja kwa msingi wa sifa na utukufu kwa Mungu. Umewahi kuwafikiria wengine kwa jinsi hii? Kwamba ile tofauti yetu kwa mtazamo wa dunia, rangi mbalimbali, dhana yetu ya 'utofauti,' imani zetu na tafsiri za kiroho zipo kwa ajili ya utukufu wa Mungu? Nimekisoma kifungu hiki mara nyingi na ninapata kipengele kwake kinachoelekeza kwenye imani yetu sisi wenyewe kuhusu wengine.

Lazima sisi tutambue kwamba jinsi tunavyo watazama wengine hudhihirisha sisi ni nani kutoka ndani ya utu wetu. Nakumbushwa kuhusu matokeo ya mawimbi unapotupa jiwe kwenye maji – kila wimbi linaungana na chanzo. Kuna uwiano kati ya matendo yetu kama waamini tunapofikiria kuhusu Warumi 15:7. Vijana wa kizazi hiki wanakua wakiwa na uelewa wa tofauti kati ya utamaduni wao wenyewe na utamaduni wa dunia wa mataifa, uhuru na teknolojia. Kwa kuwa mabadiliko ya tamaduni yapo, kwao utaifa, utamaduni na 'tofauti' vinaonekana kuwa ni nafasi ya kusherehekea na kuungana.

Je kuhusu wewe? Unaamini nini kuhusu wewe mwenyewe unachotambua kwa sababu yake Kristo amekukubali? Je, kinabadilisha jinsi unavyowatazama wengine? Je, kinashawishi jinsi unavyowatendea walio tofauti na wewe? Wewe kuwakubali wengine kumetoa utukufu kwa Mungu kwa njia zipi? Je, wewe ni chanzo cha wimbi kinachosababisha mabadiliko katika watu wa Mungu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu? Au unachangia kukatika kwa mahusiano na mtengano zaidi wa watu wa Mungu kwa sababu wao wanatofautiana?

Naamini kama watu wa Mungu lazima tuombe kwa ajili ya macho yetu ya kiroho yafunguliwe tuyaone maisha kwa jicho la Mungu – uzuri wa mataifa mbalimbali, utamaduni – na tutengeneza majukwaa ya kusifu



## JADILI:

* Mimi nina tofauti gani na watu ninaofanya kazi nao/ninaowatumikia? Je,wanamtukuza Mungu kwa sababu ya upekee wangu?
* Ni kwa njia gani mimi namtukuza Mungu kwa sababu ya utofauti wa watu wanaonizunguka?
* Warumi 15:7 inanifundisha nini kuhusu Mungu na hamu yake kwa ile huduma aliyoniitia?

na kuabudu kwa sababu ya upekee huu. Nimefurahia uzuri katika tafsiri tofauti za jamii za tamaduni tofauti zilizoonyeshwa katika vyakula, kucheza ngoma, mavazi na nyimbo, vinavyofunika mikutano yetu. Warumi 15:7 inatukumbusha sisi kuthamini tofauti hizi zaidi, tukiwachukua wengine kuwa ni njia ya Mungu inayotuelekeza kwenye kusifu na kukuza jina lake takatifu. Yote ni kumhusu yeye.

Lazima tutetee na kuongoza hizi njia za kumwabudu Mungu kupitia katika tofauti hizi, tukizungumza kwa kujiamini kuhusu utamaduni wa dunia na tuwe na bidii ya kubadilisha ukosefu wa haki wa sasa unaohusu mataifa na utamaduni ambao sio wetu. Kama mwanamke mwenye ngozi nyeusi nimepitia unyanyapaa kwa sababu ya rangi ya ngozi yangu. Uzoefu wangu huko Bangladeshi haukuhusu ubaguzi wa rangi lakini ulihusu utukufu kwa Mungu na jina lake kuwa mfano kwa sababu ya tofauti yangu. Sikuwahi hata mara moja kufikiria mimi ni msichana mweusi, lakini nilifahamu kwamba Mungu alikuwa amenituma Bangladeshi kwa sababu nilikuwa tofauti, na ni hiyo tofauti iliyokuwa inahitajika ili Mungu aweze kuonekana na kushuhudiwa na waamini wake mahali hapo.

Hivi karibuni nilitembelea Marekani wakati wa Krismasi nikaona theluji kwa mara ya kwanza. Uzuri wake kwenye miti, uwanjani na njiani vilinishangaza. Nilitamani viwanja vilivyofunikwa na theluji, na familia kadhaa zilikuwa na taa za Krismasi kupitia katika miti ya kijani zikiwa zimefunukwa kwa theluji. Ingawa nguo za kipindi cha baridi zilinifanya nionekane wa ajabu, haikuweza kulinganishwa na ule uzuri niliouona. Nilitulia nikaomba na nikampa Mungu shukurani kwa sababu ya kunipa nafasi ya kuiona dunia mpya na kupitia kwa yale ambayo marafiki zangu Wamarekani huyaona. Kwao lilikuwa jambo la kawaida, lakini kwangu ilikuwa ni nafasi na uzoefu niliopewa na Mungu. Muujiza wa namna hii kutoka kwa Mungu uliweka ibada ndani ya roho yangu na ushuhuda wa kuwaambia marafiki zangu wa Kenya. Nimeona vile vile dhihirisho la kufanana na hili wakati nimekuwa mwenyeji wa marafiki huko Kenya nikawapeleka kwenye kituo cha Twiga. Mshangao kwenye nyuso zao haukuwa na kiwango cha fedha na ushuhuda wao juu ya uumbaji wa Mungu ulivyo wa ajabu, vinanikumbusha nitulie na kushukuru kwa yale ambayo ni ya kawaida kwangu.

Fundisho hili katika Warumi 15:7 ni fundisho tunalotakiwa kulikumbatia, likitukumbusha kuzikubali tofauti zetu za utaifa na utamaduni. Katika tofauti zetu, Kristo bado anatukubali. Kwa kutambua hili, tunatakiwa kumhukumu kila mmoja?

Fikiria kuhusu maisha, kazi yako na tofauti za watu ambao Mungu amekupa. Mungu kwa makusudi amekuweka mahali ulipo. Ameweka tofauti kukuzunguka kwa ajili ya utukufu wake na udhihirisho wa ukuu wake.

Baba, katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo, nakushukuru kwa ufunuo wa neno lako, kwamba uumbaji wako wote na uzuri wa tofauti zilizopo vyote vinahusu kukupa wewe sifa, utukufu na heshima. Naomba kwa ajili ya hekima ya kupeleka baraka na ufunuo huu kwa wale ambao wanategemea niwaongoze. Katika jina la Yesu naomba. Amina.

**MEBLE VILIKA BIRENGO**
KENYA MASHARIKI
Meble Vilika Birengo ni Mtaalamu wa Mguso na Mafunzo wa Tume ya Kimataifa ya Haki za Jamii. Mtoto wa saba wa marehemu Mameja Daniel na Mary Birengo, yeye ni askari wa Nairobi Central Temple naye ana shauku ya maendeleo ya kiroho na uongozi. Yeye ni mpiga tromboni, mezzo soprano kiongozi huko Kenya Conservatoire of Music Nairobi. Ana shahada ya BSc katika Uongozi na Utawala, shahada ya pili (MA) katika Ufatiliaji na Tathmini.



# WENGINE NA UPATIKANAJI

LUKA 14:13-14

MEJA NANCY HELMS

'Bali ufanyapo karamu waite maskini, vilema, viwete, vipofu nawe utakuwa heri, kwa kuwa hao hawana cha kukulipa, kwa maana utalipwa kwenye ufufuo wa wenye haki' (Luka 14:13-14).


## 'WENGI HAWAPO KWENYE MEZA KATIKA UFALME WA MUNGU KWA SABABU KANISA HALIJATOA NJIA YA KUFIKIA HUKO.'

Labda haitakushangaza kujifunza kwamba wenye ulemavu ndilo kundi kubwa la waliotengwa duniani na katika Kanisa. Limekuwa ndilo jambo muhimu la haki ya jamii kabla ya Yesu kutembea katika dunia hii, na ni jambo ambalo alilishughulikia kwa nguvu na nia, tena na tena katika injili. Mara nyingi aliwakumbusha wasikilizaji wake waache nafasi katika maisha yao kwa ajili ya wengine waliomo duniani – waliotengwa, walionyamazishwa, na kukataliwa.

Sisi bila shaka tunawafahamu watu walio katika jamii zetu wenye ulemavu walio na upweke, walionyamazishwa na wanaotamani kuwa sehemu ya popote. Katika Marko 10:46-52 tunasoma habari za mtu mmoja wa namna hii aliyeita apate msaada huku akipuuzwa, akitulizwa na kusukumwa kwenda mwisho wa wale ambao hawana muda, hawana uvumilivu au huruma. Bartimayo, kutoka Yeriko, alikuwa kipofu, na ulemavu wake mara moja ulimwekea alama ya kufukuzwa. Hakuwa sehemu ya - popote. Kama ulemavu mwingi siku hizo, alikuwa na mahali pake pa siku zote pa kuombea msaada, ili tu aweze kuishi. Siku moja ya muujiza, mahali pake pembeni mwa barabara palithibitisha kuwa mahali pa kubadilisha maisha na kutoa maisha.

Marko 10:47 inasema, 'Naye aliposikia ya kwamba ni Yesu Mnazareti, alianza kupaza sauti yake, na kusema, mwana wa Daudi, Yesu, unirehemu.!"' Kwa kumwita 'Mwana wa Daudi', yule mtu kipofu alithibitisha anafahamu kwamba Yesu ni Masihi. Kilio chake kiliwachosha waliokuwa wamesimama kuzunguka, waliofikiri bila shaka, kwamba yuko nje. Walifanya wawezavyo kumtuliza, lakini alivumilia na akaendelea kupaza sauti hata zaidi, '"Mwana wa Daudi, unirehemu!"' Yesu alisimama! 'akasema mwiteni', (Marko 10:49). Wanafunzi wakamwita – akisimama kwa miguu yake alienda kwa Yesu. Yesu alimuuliza swali rahisi, 'Wataka nikufanyie nini?' (mst 50). Kwa imani, Bartimayo alimpa jibu rahisi, 'Mwalimu, nataka nipate kuona' (mst 51). Angeweza kumwomba Yesu chochote ambacho kingempa mahitaji na kumfanya awe sehemu ya popote. Yesu alimponya, naye akamfuata Yesu njiani.

Watu wengi wanaweza kusema kwamba uponyaji wake kimwili wa kuona kwake ulikuwa ndiyo tendo dhahiri zaidi lililofanyika walipokutana. Hebu tufikirie kwamba Bartimayo kuweza kuungana na kundi na kumfuata Yesu lilikuwa labda ndilo jambo kuu la wakati huo na katika maisha yake. Ilikuwa ni kama mara ya kwanza kwake kuwa hajatengwa katika muda mrefu, aliyetupwa pembeni. Ghafla alikuwa na uwezo wa kuwafikia wale walio katika jamii ambao huko nyuma walikuwa wamemkataa. Kurejeshwa kwa kuona kwake kulimaanisha sasa anaweza kuwa sehemu ya jamii. Fikiria juu ya uponyaji wa hisia na roho alioupata wakati huo. Inamfanya mtu ajiulize watu wangapi leo wenye ulemavu wangependa kujiunga na wengine na wamfuate Yesu lakini hawajapewa nafasi na njia na wale walio Kanisani.



## JADILI:

* Unaweza kuwataja majina watu wenye ulemavu katika kanisa katika jamii yako walio na nafasi dhahiri kwenye meza? Unaweza kuwataja wale ambao wanakosekana mezani?
* Ni kwa njia zipi bila kukusudia tunawanyamazisha watu wenye ulemavu? Ni kwa namna gani tunaweza kuwapa sauti?
* Tunamfahamu nani mwenye ulemavu ambaye tunaweza kumuuliza swali, 'unataka nikufanyie nini?'

Katika Luka 14:12-14, Yesu anawahutubia Mafarisayo. Walipenda sana kuwa na viti vya upendeleo na kualika wageni mashuhuri kwenye tafrija zao. Yesu aliangalia pote kwenye meza akagundua jinsi ambavyo wageni walichagua nafasi za heshima. Akamwambia mwenyeji, ' "Ukitoa chakula cha mchana au cha jioni, usialike marafiki zako, kaka au dada zako, ndugu zako, au majirani zako matajiri; ukifanya hivyo wanaweza kukualika kwao vile vile na kwa hiyo utakuwa umelipwa. Lakini ukitoa sherehe, waalike maskini, walemavu, na vipofu nawe utabarikiwa. Ingawa hawawezi kukulipa, utalipwa kwenye ufufuo wa wenye haki. " ' Wengi hawapo mezani katika ufalme wa Mungu kwa sababu Kanisa halijawapa njia ya kufika hapo.

Debie Thomas, katika makala inayoitwa, 'Tabia za Mezani - Table Manners', inasema, 'Tutakapo thubutu kukusanyika kwenye meza ya Yesu', kwa vitendo tunapinga desturi ya mwendo wa kwenda juu na ushindani unaotuzunguka. Hakuna lililo rahisi au la moja kwa moja linalotuzunguka. Halipo lililo rahisi kuhusu hili; linahitaji kazi kubwa kwa muda mrefu. Kula na kunywa pamoja na Mungu ni kuishi katika mvutano na utaratibu unaolezea vyumba vyetu vya mikutano, mabaraza yetu, siasa za kanisani kwetu – na hilo linaweza kuchosha. Lakini ndilo tuliloitiwa kulifanya – kujinyenyekeza na kuweka matumaini yetu kwenye ufalme mwingine mkali... Pale tunapokaa huzungumza kwa uzito sana, na watu tunaochagua kualika hudhihirisha yaliyomo ndani ya nafsi zetu.' Fikiria unavyoweza kutoa uponyaji wa kihisia na kiroho kwa 'wengine', kwa kutoa nafasi za mahali pa wao kujisikia ni sehemu yake.

Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, tunapoielekeza mioyo yetu kwako, tusaidie tuzigeuze meza zetu kwa wengine.



**MEJA NANCY HELMS**

MAREKANI MAGHARIBI

Meja Nancy Helms ni mama wa wanne, bibi wa wanne, kipenzi cha bahari, mjuzi wa chokoleti, na kazi endelevu. Yeye ni afisa wa Jeshi la Wokovu kwa sasa anatumika kama Afisa wa Teritori wa Msaada wa Malezi ya Kiroho na Mkurugenzi wa Teritori wa Huduma za Walemavu katika Teritori ya Marekani Magharibi. Mtoto wake wa pili, Cameron, aliye na ulemavu, ndiye shujaa wake maishani naye amechukua nafasi kuu katika maisha yake akisaidia kumfahamisha kuhusu mjumuisho na kuwa sehemu ya dunia na Kanisa. Amemuonyesha kwamba kitu pekee kilicho cha muhimu ni imani inayojionyesha yenyewe kupitia kwa upendo.

# WANAFUNZI WANAOZAA MATUNDA

1 WAKORINTHO 13:5

MEJA RACHEL KANDAMA

'Upendo huvumilia, hufadhili, upendo hauhusudu, upendo hautakabari, haujivuni, haukosi kuwa na adabu, hautafuti mambo yake, hauoni uchungu, hauhesabu mabaya,' (1 Wakorintho 13:4-5).

Upendo usio na ubinafsi siku zote huwafikiria wengine. Kama tukitumia kanuni ya upendo usio na ubinafsi katika familia zetu, nyumba zetu zitakuwa huru kutokana na migongano na zitamheshimu Yesu Kristo ambaye hakuja kutumikiwa, bali kutumika na kuyatoa maisha yake sadaka kwa wengi.

Maisha ambayo yamejitoa hayataki kuwatumikia wengine hatimaye yatapoteza maana yake. Mungu alituumba tutumike, ameyafuma hayo kama nyaya ndani ya mioyo yetu kutaka kutumika na kuwa na kusudi ambalo ni kubwa zaidi ya kuishi tu kwa ajili ya wengine.

'Siku moja Petro na Yohana walikuwa wanakwenda hekaluni wakati wa maombi saa tisa mchana. Mtu mmoja mlemavu kutoka kuzaliwa alikuwa anabebwa kupelekwa kwenye lango la hekalu lililoitwa Mzuri, alipokuwa akiwekwa kila siku aombe msaada kutoka kwa wale waliokuwa wakiingia hekaluni. Alipowaona Petro na Yohana karibu waingie, aliwaomba fedha.

'Na Petro akamkazia macho, pamoja na Yohana akasema, tutazame sisi. Akawaangalia akitarajia kupata kitu kutoka kwao, lakini Petro akasema, mimi sina fedha, wala dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho nikupacho. Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti , simama uende. Akamshika mkono wa kuume, akamwinua, mara nyayo zake na vifungo vya miguu yake vikatiwa nguvu. Akaondoka upesi akaanza kwenda, akaingia ndani ya hekalu pamoja nao, akienda akiruka ruka, na kumsifu Mungu.' (Matendo 3:1-8).

Unakutana na watu wangapi kila siku wanaopitia katika nyakati za changamoto nao wanatumaini mtu mmoja atatambua na atajitoa awasaidie?

Jambo la kwanza alilolifanya Petro lilikuwa kusimama na akamfanya yule mlemavu awatizame yeye na Yohana. Tendo hili lilimweka yule mtu katika nafasi ya usawa na wao. Marafiki, kama mnatafuta kuwa wanafunzi wanaozaa matunda lazima muwafikie wengine binafsi na lazima muwe na roho ya kujumuisha, bila kujali hadhi na rangi yake.

Jambo lililofuatia ambalo Petro alilifanya ni kumwambia yule mlemavu kwamba ingawa hakuwa na fedha, atampa kile alicho nacho. Alikuwa na nini? Alikuwa na Yesu Kristo. Sisi tuna nini ambacho tunaweza kuwapa wengine? Tunaweza kuwa katika nafasi ambayo Petro na Yohana walijikuta ndani yake ya kutokuwa na fedha wala dhahabu, lakini tunaye Yesu ndani yetu ambaye tunaweza kuwapa na wengine ambao bado hawajampokea kama mwokozi wao binafsi.

## HUDUMA BINAFSI KWA WENGINE

Shughuli za maisha yetu, hata shughuli zetu za kila siku, hazitakiwi kuonekana kuwa hazina umuhimu; zinachangia kwa namna ambayo Mungu anataka kututumia.

Wakati mwingine tunajisikia hatuna vya kutosha kuwagawia wengine, lakini kuwafikiria wengine kunahitaji tu kuwa na utayari na utii, ili tuthamini mahitaji ya watu wengine zaidi ya yale ya kwetu.

Matukio ya maisha ni vyombo na mawakala wa Mweza yote kwa hiyo lazima tufikirie, tuamini na tutende ipasavyo. Inahitaji vile vile akili zetu zielekee mwelekeo wa Mungu na tumtegemee yeye jumla. Katika 1 Wafalme 17:8-16, mjane alimwamini Mungu hata katika kile kidogo alichokuwa amebakia nacho. Kutokana na kitendo chake, Mungu akampa vingi: 'Basi akaenda...akafanya kama alivyosema Eliya, na yeye mwenyewe, na Eliya, na nyumba yake, wakala siku nyingi. Lile pipa la unga halikupunguka, wala ile chupa ya mafuta haikuisha sawasawa na neno la Bwana alilolinena kwa kinywa cha Eliya' (mst. 15-16).



**JADILI:**

* Unafanya kazi na nafsi ngapi zilizopotea na huchukui muda wa kuwaambia kuhusu Yesu?
* Umewahi kufikiria kwamba kabla Mungu hajakutana na mahitaji yako, au katika kukutana na mahitaji yako, anataka kukutumia kukutana na mahitaji ya wengine?

Mungu hutumia kukutana huku kukamata usikivu wetu, kubadilisha vile tunavyo vithamini, mienendo, vipaumbele, ufatiliaji na kubadilisha vyanzo vyetu vya imani ya usalama na furaha. Hebu tusikose kuona kwamba tukio lile lile linalotujaribu mara nyingi huja likawa njia ambayo Mungu anaweza kututumia katika huduma kwa wengine. Hitaji la Eliya likawa njia ya kukutana na mahitaji ndani ya maisha ya mjane na mtoto wake.

## 'UKITAFUTA KUWA MWANAFUNZI ANAYEZAA MATUNDA LAZIMA BINAFSI UWAFIKIE WENGINE NA LAZIMA UWE NA ROHO YA KUJUMUISHA, BILA KUJALI HALI AU TAIFA LA MTU.'

Hii inatukumbusha kwamba hatupo hapa kwa ajili yetu wenyewe, lakini tupo kwa ajili ya wengine vile vile.

Kufanana na Kristo maana yake ni kwamba hata katika maumivu yetu tunatakiwa kuwafikiria wengine na jinsi Mungu anavyotaka kututumia. Tunaweza tukajikuta tumo katika jamii ambayo inazingatia lile ambalo ni muhimu kwa ajili yangu, bila kuwajali wengine. Ni kuhusu nini ni bora zaidi kwa ajili ya kazi yangu, furaha yangu, usalama wangu, umuhimu wangu. Kuwafikiria wengine kunahitaji tusitizame tu mahitaji yetu wenyewe lakini tuyatizame mahitaji ya wengine vile vile.

Yesu anatuita tumfuate kwenye maisha ya kuwatumikia wengine.



Mpendwa Bwana Yesu, tusaidie tuwe na roho sahihi kama wanafunzi wako katika kuwafikia watu bila ya ubaguzi. Tusaidie tuwe na moyo unaowapa wengine kipaumbele kwanza, kwani mara nyingi tumeshindwa kuona mahitaji ya wengine. Bwana, tusaidie tuishi kulingana na kiwango cha upendo wako tunavyojitahidi kuwatumikia wengine. Amina.

**MEJA RACHEL KANDAMA**
ZAMBIA
Meja Rachel Mwiinga Kandama alitawazwa kuwa afisa mwaka 2005 wa kundi la Wana Maono. Ametumika kikaoni, chuoni, Makao Makuu ya Teritori na kwenye maagizo ya sehemu. Sasa anatumika kama Katibu wa Teritori wa Vijana na Watakaji. Rachel ana diploma ya kazi ya jamii, na ameolewa ana watoto watatu: Kalinda, 17; Joshua, 7; na Emmanuel, 3. Anapenda kuimba na kucheza muziki wa injili.



# TUMAINI NYAKATI NGUMU

AYUBU 1:1-3, 13-22; AYUBU 2:1-13

MEJA ROBIN BLACK

Ayubu alikuwa na maisha mazuri, akiwa na watoto 10, marafiki wazuri, afya njema na utajiri mkubwa. Siku moja alipoteza vyote. Kwa kweli, hakupoteza vyote, mkewe mpendwa alikuwa bado karibu naye. Ungetegemea kwamba atakuwa tumaini kwake Ayubu. Lakini mke wa Ayubu alisema, 'Je, wewe hata sasa washikamana na utimilifu wako? Umkufuru Mungu ukafe!' (Ayubu 2:9).

Hakuwa mtu wa kutia moyo! Labda sisi tuwe na huruma kwa mke wa Ayubu, hata hivyo, hata yeye alikuwa amewapoteza watoto wake, mji wake na utajiri wake. Anaweza kuwa alikuwa anajibu hivyo dhidi ya Mungu kwa sababu ya maumivu yake mwenyewe.

Ayubu vile vile alikuwa na marafiki watatu wa kumsaidia. Jambo la kwanza walilolifanya lilikuwa kukaa naye kwa ukimya. 'Kisha wakaketi nchi pamoja naye muda wa siku saba, mchana na usiku, wala hapana mmoja aliyenena naye neno lolote, kwa maana waliona ya kuwa mashaka yake aliyo nayo ni makuu mno.' (Ayubu 2:13).

Wakati mtu tunayemfahamu amepitia huzuni, hasa hasara kubwa isiyotarajiwa, tunaweza kujiuliza ni maneno gani ya faraja tunayoweza kumpa. Lakini hatulazimiki kusema chochote. Kama marafiki wa Ayubu, huduma ya kule kuwepo kwao tu ilikuwa huduma yenye nguvu sana. Kusikiliza habari ya maumivu na uchungu inaonyesha kwamba unajali. Kustarehe katika ukimya hutoa nafasi kwa Roho Mtakatifu kutunong'oneza.

Jambo lililofuata ambalo marafiki zake Ayubu walilifanya lilikuwa ni kumtia moyo: 'Maneno yako yamemtegemeza huyo aliyekuwa anaanguka, nawe umeyaimarisha magoti manyonge' (Ayubu 4:4).


Walikuwa wanasema 'Najua mambo sio mazuri sasa, lakini kumbuka kiasi gani uliwasaidia watu huko nyuma'. Unapokuwa unamhudumia mtu ambaye moyo wake umeshushwa sana, inaweza kusaidia kuwakumbusha nyakati za nyuma wakati mambo yalitimizwa na Mungu alikuwa anatenda kupitia kwao ili kuwasaidia wengine. Wakati mwengine kuyakumbuka ya nyuma kunaweza kuleta faraja na kutia moyo. Inaweza kutukumbusha kwamba maisha hayakuwa siku zote ni magumu na kwamba kuna tumaini la siku zijazo.

Kisha marafiki zake Ayubu walimpa ushauri: 'Lakini mimi ningemtafuta Mungu, ningemwekea Mungu dawa yangu' (Ayubu 5:8).

Marafiki zake Ayubu wanamwambia akate rufaa au amwombe Mungu. Tunapo wahudumia watu ambao wameshushwa mioyo au wana msongo wa mawazo, tuna utajiri wa ajabu mbinguni tunaoweza kuutumia. Tunaweza kwa taratibu tukawakumbusha marafiki zetu kwamba wanaweza 'Huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu' (1 Petro 5:7). Mara nyingi maombi yameleta faraja na amani kwa mtu anayepitia wasiwasi, mashaka na kushushwa moyo.

Kwa wakati huo, huu ndiyo ulikuwa ukweli wa Ayubu: 'Hapo nilalapo chini, nasema, "Nitaondoka lini?" Lakini usiku huwa mrefu, nami nimejawa na kujitupa huku na huku hata kupambazuke…ninadhoofika, sitaishi siku zote, usinisumbue, kwani siku zangu ni uvuvio.' (Ayubu 7:4, 16).

Ayubu anapitia usingizi wa kutaabisha, akijitupa na kujigeuza huku na kule, huzuni nzito, akilala bila kupata usingizi, akiwa na mashaka na hali yake usiku mzima, akitaka awe peke yake, akijisikia kwamba maisha hayana maana au kusudi. Hizi zinaweza kuwa baadhi ya dalili za huzuni, kupoteza, msongo wa mawazo au shauku. Watu wengi hupitia haya katika maisha yao. Ayubu anatuonyesha namna ya kushughulika na matatizo haya.



## JADILI:

* Jadili kuhusu majibu ya mke wa Ayubu na marafiki zake. Nini kilisaidia? Nini kilikuwa hakisaidii? Ungeweza kumsaidia namna gani mtu ambaye anapitia mazingira magumu, wakati ameshushwa moyo sana?
* Una rafiki ambaye yuko katikati ya mazingira magumu sana hivi sasa? Unaweza kumwombea na ukate rufaa kwa Mungu kwa niaba yake?
* Huenda wewe unapitia nyakati za kuwa na wasiwasi au msongo wa mawazo, na unajisikia kwamba maisha hayana maana? Kuna mtu fulani, rafiki wa kuaminika kama aliyekuwa naye Ayubu, ambaye unaweza kuongea na kuomba naye? Kumbuka, Mungu anataka tumtwishe yeye mizigo yetu yote, kwa sababu yeye anatujali.

Hata katika kukata tamaa kwake, Ayubu hamwachi Mungu. Ingawa anajisikia kwamba maisha yake hayana kusudi wakati huo, Ayubu bado anamng'ang'ania Mungu kwa sababu maisha yake yanategemea hilo. Akizungumza kuhusu Mungu anasema, 'Tazama, ataniua, sina tumaini, ila hata hivyo nitaithibitisha njia yangu mbele yake.' (Ayubu 13:15).

Ayubu anaelewa tumaini linatoka wapi. Watu wengi hupitia maumivu na kushushwa mioyo maishani, na wakati mwingine hupoteza kumtumaini Mungu. Wanafikiri Mungu hawajali na mambo yao. Lakini tukisoma injili, tunaona Yesu mara nyingi anasukumwa na huruma kwa watu. Tunapomwona Yesu akilia kwenye kaburi la Lazaro, tunaona sura ya Mungu anayeyasikia maumivu yetu. Ingawa tunapitia kukatishwa tamaa na uchungu hii haina maana kwamba Mungu hajali. Maumivu yetu maana yake ni kwamba tunaishi katika dunia yenye ugonjwa nayo imevunjika, na Mungu hata yeye ameshushwa moyo nayo.

Wakati akiwa bado katikati ya mazingira yenye kuangamiza Ayubu alisema, 'Lakini mimi najua ya kwamba mtetezi wangu yu hai, na yakuwa hatimaye atasimama juu ya nchi. Na baada ya ngozi yangu kuharibiwa hivi, lakini pasipokuwa na mwili wangu nitamwona Mungu' (Ayubu 19:25-26).

Hii kweli ni kauli ya imani – chochote kinachotendeka katika maisha yangu, najua kwamba mtetezi wangu yu hai! Na hata kama huu mwili wa uharibifu ukiharibiwa, nitaishi naye. Mungu ametumia maisha ya Ayubu kuwahudumia watu wanaopita katika nyakati za giza Atahudumu kupitia katika maisha yetu, hata wakati wetu wa giza nene, kama tutashikilia tumaini katika Yesu.

**'TUNAPO WAHUDUMIA WATU AMBAO WAMESHUSHWA MIOYO AU WANA MSONGO WA MAWAZO, TUNA UTAJIRI WA AJABU MBINGUNI TUNAOWEZA KUUTUMIA.'**

Baba wa Mbinguni, tunashukuru kwamba unatufahamu na unatujali. Wewe ndiye tumaini letu kwa sababu tunajua mtetezi wetu yu hai! Amina.

**MEJA ROBYN BLACK**
AUSTRALIA
Meja Robyn Black ni afisa wa kikao cha Auburn na afisa wa eneo huko Sydney. Robyn anapenda watu na anampenda Yesu, na anaamini haipo raha kuu maishani kuliko kuhudumu katika jina la Yesu.



# MKAO WA MWANAMKE

LUKA 13:10-17

MEJA SARAI ORTIZ

Sinema ya *Nje Ndani* (*Inside Out)* inaonyesha hisia mbalimbali za Riley mwenye umri wa miaka 11: furaha, hofu, na hasira. Anapoonyesha kukatishwa tamaa, anakuwa anaongozwa na hisia. Mwonekano wa nje hutoa sura ya hali ya ndani. Hofu, kukatishwa tamaa, msongo wa Mawazo, mambo tunayokabiliana nayo na kuyabeba, mara nyingi hutufanya tuelekee kwenye msimamo wetu. Tunayaona haya katika mwanamke aliye katika Luka 13:10-17.

### MWANAMKE ALIYEPINDA (LUKA 13:11)

Kwa miaka 18 mwanamke huyu alikuwa amepinda, amelemazwa na pepo. Mkao wa mwili wake ulibeba hisia za msongo wa mawazo, kutengwa, aibu na kujiona wa chini. Ni mara nyingi kiasi gani tumejisikia hivyo wakati matatizo yametusonga, tunapojilinganisha na wengine? Lakini baada ya miaka 18, wakati wa utukufu wa kukutana na Yesu uliwadia.

**'MATOKEO YA UPONYAJI WA MUNGU HUENDA ZAIDI YA HALI NJEMA YA KIMWILI; NI UPONYAJI WA ROHO NA HISIA.'**

### YESU ANAWAJALI WENGINE (LUKA 13:12-13)

A. Yesu 'aliona'. Bila kujali watu wangapi walikuwa wamemzunguka Yesu, aliona mahitaji ya mwanamke huyu. Tunaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu anatujali naye huona mahitaji yetu naye anahusika na utatuzi wa mateso yetu.

B. Yesu 'alimwita'. Ingawa Biblia haitaji jina lake, yeye alimwita; hilo ni la muhimu. Bwana anapotuita, anatufahamu ana muda na sisi katika mashaka yetu ya kila siku. Basi hebu tupumzike katika Mungu ajuaye yote.

C. Yesu 'alimwambia'. Katika kuzungumza naye, anamsikiliza mwanamke aliyeonekana kuwa ana umuhimu mdogo nyakati hizo. Mungu huzungumza nasi siku hizi kupitia kwenye Biblia, akitupa faraja na kututia moyo nyakati za majaribu. Hebu tulitizame neno lake tujazwe nguvu zake.

D. Yesu 'alimgusa'. Anakwenda hatua moja zaidi ya kuona, kuita na kusema; anaweka mikono yake juu yake. Mguso uliobadilisha maisha ya mwanamke huyu jumla. Ni wangapi wetu tumejisikia kuguswa kwa njia maalum namna hiyo na Bwana wetu? Ni kwa kumkaribia Yesu ndipo tutakapoweza kuusikia mguzo wa namna hiyo. Kwa hiyo, sisi pia, tunaweza kuyagusa maisha ya wengine ili kuwabariki.

E. Yesu 'alimponya'. Hatatembea akiwa amejikunja tena; umbo lake lilibadilika, alinyooka, usoni alidhihirisha furaha na mshangao, na alianza kumtukuza na kumsifu Mungu. Ile aibu ikabadilika kuwa furaha, kuwa wimbo. Matokeo ya uponyaji wa Mungu huenda zaidi ya kuwa sawa kimwili; ni uponyaji wa kiroho na wa kihisia.



## JADILI:

* Fikiria kuhusu miujiza na maajabu katika maisha yako, na wakati ulijibiwa maombi. Lini ilikuwa mara ya mwisho wewe kumshukuru Bwana kwa yote aliyokutendea?
* Fikiria ulivyosimama. Ni taswira ya kweli ya kazi iliyofanyika ndani?

### WATU WA DINI WENYE UCHOYO NA HASIRA (LUKA 13:14-17)

A. Kiongozi wa sinagogi alikuwa mwenye hasira kwa sababu Yesu alikuwa ameponya mtu siku ya Sabato. Alikuwa na msimamo wa kwake mwenyewe. Watu wengine siku zote watakataa kufumbua macho yao ya kiroho nao watakuwa wapinzani wa Mungu na watu wake.

B. Walizifanyia kazi thamani zisizo sawa. Ni muhimu zaidi kuwajali wengine na mahitaji yao kuliko kuheshimu Sabato. Yesu alisema. Kama ng'ombe au punda anaweza kupelekwa kunywa maji siku ya Sabato, kwa nini basi mwanamke asiwekwe huru kutokana na kile kilichokuwa kinamfunga?

C. Waliona aibu. Yesu alitumia maneno mazito dhidi ya wapinzani wake: 'Ninyi wanafiki!' Yesu analinda nafasi ya mwanamke huyu, anawaaibisha maadui kwa mamlaka, anawadhalilisha mbele ya watu, 'lakini watu walifurahishwa na mambo yote mazuri aliyokuwa anayafanya'.

Tuwashirikishe wengine maajabu na miujiza ya maishani mwetu. Fikiria ni maajabu mangapi ambayo Mungu ameyafanya maishani mwako: alipojibu maombi yako ya kuhitaji uponyaji, alipokupa mahitaji yako wakati wa upungufu, alipokupa kazi. Alikulinda katika ajali ile alipoleta faraja katikati ya shida na akakupa amani katikati ya dhoruba. Umemtambua? Umemshukuru? Umemsifu? Kama unajikuta bado umepinda, katika wasiwasi na mahitaji yako, nakualika umtizame Yesu, sikiliza sauti yake na usikie mguso wake wa upendo.



Baba, natambua nguvu ya upendo wako kwangu; unaniita kwa jina langu kwa sababu unanifahamu, unayafahamu mahitaji na mahangaiko yangu. Unafahamu dosari zangu, Na bado unanipenda na kunisamehe mimi. Niongoze kwenye ushindi kwa uwezo ambao ni wewe tu unayeweza kunipa. Natambua kwamba ni wewe tu unayeweza kunipa amani, hekima na ushirika ninapojisikia kuwa mpweke, na siku zangu zijazo chini ya usimamizi wako. Ninapoamka, naomba iwe ni kukusifu wewe, kuwatumikia wengine na kukuheshimu wewe kwa matendo yangu, nikimfikiria yeye anayetakiwa kukusikiliza na kuguswa na wewe. Katika jina la Yesu. Amina.

### MEJA SARAI ORTIZ

MEXICO

Nimetumika kama afisa pamoja na mume wangu kwa miaka 25; sisi ni sehemu ya kundi la Wajumbe wa Upendo wa Mungu. Katika agizo langu la sasa natumika katika Hifadhi ya Wahamiaji huko Tijuana kaskazini ya Mexico kwenye mpaka na Marekani. Mimi ni mama wa watoto wanne wanaomfahamu Yesu kama Mwokozi wao nami nafurahi sana kuwa bibi wa wajukuu wawili wa kike. Nilishawishika na mfano wa maisha ya wazazi wangu wastaafu na miaka yao 39 ya utumishi.



# KIBURUDISHO CHA UKARIMU KWA WOTE !

MITHALI 11:25

MEJA TRACY BRIGGS

## ' "WENGINE" – NI MAELEZO YA MAISHA YA YESU, MFANO KWA AJILI YETU KUUFUATA.'

'...anyweshaye atanyweshwa mwenyewe' (Mithali 11:25)

Bahari ya Galilaya inapatikana Kaskazini ya Israeli. Bahari hii ina uhai wa wanyama na maisha ya mimea. Watu wamekuwa wakivua kutoka katika maji haya kwa miaka elfu nyingi. Ni bahari yenye uhai. Hata hiyo, karibu kilomita 105 kusini kuna Bahari ya Chumvi (bahari iliyokufa). Bahari ya chumvi ina chumvi karibu mara tisa zaidi ya bahari ya kawaida. Chumvi hii inafanya mazingira yawe magumu sana kiasi kwamba wanyama na mimea haiwezi kuishi.

Kwa nini moja imejawa na uhai wakati ile nyingine inajulikana kuwa ni bahari ya chumvi (bahari iliyokufa)? Bahari ya Galilaya inashibishwa kutoka kaskazini na baadaye hutiririka katika mto Yordani. Maji huja ndani, na maji hutoka. Lakini, Bahari ya Chumvi yenyewe hupokea maji yanayoingia tu na hayatoki.

Bahari moja hupokea na kutoa. Ile nyingi hupokea peke yake.

Tunafahamu ukweli huu kwa miili yetu. Ikiwa kile ninachoingiza ndani ni zaidi ya nguvu ninazotumia, basi najua nina tatizo. Nitaongeza uzito na inaweza kusababisha nikawa na shinikizo la damu, moyo usio na afya njema, mafuta mengi n.k. Natakiwa kuwa natoa, nafanya mazoezi na kutumia misuli yangu. Ndipo nitakapokuwa na afya na mwenye nguvu. Kama nitakuwa naingiza tu, nitaugua, lakini nikitoa napata afya.

Katika dunia ya asili tunaona kujitizama mwenyewe huleta kifo, giza na magonjwa wakati katika kutoa kuna uhai, mwanga na afya. Sio tu kwamba hii ni kanuni ya asili lakini ni kanuni ya kiroho tuliyopewa na Mungu.

Tunaona hili katika hali iliyokithiri katika Yesu katika Wafilipi 2:6-11: 'ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana namna ya wanadamu, tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam mauti ya msalaba. Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba.'

'Wengine' – ni utambulisho wa maisha ya Yesu, mfano wetu wa kufuata. Mara nyingi tena tunasoma katika maelekezo ya Mungu kwa Kanisa la mwanzo, kwa wale ambao watafuata mfano wa Yesu wa kuhusika na wengine wa vizazi vyote. Vijana, wazee na walio kati, tumeitwa kuwa hudumia wote kama Yesu alivyofanya. Tazama vifungu hivi: Wafilipi 2:4; 1 Wakorintho 10:24; Waefeso 5:21; Mathayo 20:28. 'Wengine' ni kuishi maisha mazito. Sio rahisi. Ni kukabiliana na utamaduni kwa sababu tunaishi katika dunia ambayo imejinyonya yenyewe. Kujipenda sana, haki zangu, faraja yangu.

Ni changamoto kwetu kuwa 'wanaozingatia wengine'. Na bado kuna ahadi ya nitakapo wafurahisha wengine, najifurahisha mwenyewe. Jina moja ambalo Mungu alijulikana kuwa ndilo jina lake siku za zamani lilikuwa ni El Roi – Mungu aonaye. Mungu wetu hutuona. Naye anaahidi kuwazawadia wale ambao huishi kwa ajili ya wengine (Zaburi 149).



## JADILI:

* Umenufaika kwa njia gani kutokana na kumsaidia mwingine?
* Yesu aliachana na nafasi ipi ya upendeleo wa Mungu? Yesu alitoa nini kwa ajili yako? Majibu ya Mungu yalikuwa ni yapi?
* Ni kwa njia zipi wewe huonyesha tabia za uchoyo? Unayashinda hayo kwa namna gani?
* Ni ipi njia moja unaweza kutumia ujuzi, maarifa, vitu ulivyo navyo, upendo au muda kwa ajili ya wengine wa vizazi vyote juma hili?

Mathayo 10:42: 'Na mtu awaye yote atakayemnywesha mmoja wapo wa wadogo hawa ngaa kikombe cha maji ya baridi, kwa kuwa ni mwanafunzi, amini, nawaambia, haitampotea kamwe thawabu yake.'

Luka 6:35: 'Bali wapendeni adui zenu, tendeni mema, na kukopesha msitumaini kupata malipo, na thawabu yenu itakuwa nyingi; nanyi mtakuwa wana wa aliye juu, kwa kuwa yeye ni mwema kwa wasio mshukuru, na waovu.'

Tunapo mfahamu na kuwa na uzoefu wa Yesu katika maisha yetu tunaweza kuwajali wengine, hatufanyi hivyo kutoka mahali pa mapungufu bali kutoka mahali pa usalama, utajiri, palipojaa na upendo. Bahari ya Galilaya inatiririka kutokana na kujaa kwake na tunaweza kuwapenda wengine kutoka mahali pa sisi kupendwa, tukiwa na tumaini na kufahamu sisi ni mali yake Mungu. Kwani tunaye Mungu anayetuona, nasi tutaburudishwa tunapowaburudisha wengine.



Bwana Yesu nionyeshe leo wale ambao naweza kuwaburudisha na unisaidie niwe na ujasiri wa kuchukua hatua. Katika jina la Yesu. Amina.

**MEJA TRACY BRIGGS**
AUSTRALIA
Nimekuwa katika ndoa kwa miaka 30 na mtu wa Mungu, mcheshi, mtu wa ajabu. Tuna watoto watatu wazuri, mabinti wawili na mvulana mmoja, na mke wa mwanetu na mume wa binti yetu wa ajabu. Tuna mjukuu wa kiume maridadi wa miezi 18 ambaye ni baraka kweli! Mume wangu nami tumekuwa maafisa kwa miaka 27 nasi twapenda kumtumikia Mungu pamoja. Mimi ni afisa wa eneo huko New South Wales Kaskazini.



# UTOFAUTI WA VIZAZI

KAPTENI WILLEKE VAN DER WOUDE-VAN DE VENIS

1 WAKORINTHO 12:27

'Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake' (1 Wakorintho 12:27). Kifungu hiki cha Biblia ni cha kawaida na cha haki – kinachotumika kuelezea kwa nini kanisani tunatakiwa kuwa wenye kujali karama zinazotolewa na Roho kwa kila mmoja: kila mmoja anathaminiwa na kutunzwa, kwa sababu karama zake zimetolewa kwa kusudi la kusaidia Kanisa lifikie ukamilifu wake.

Kuna mipango yenye maswali ya kuhojiana kwa kina kutusaidia tujue kuhusu karama zetu za rohoni. Kwa wengine, mipango hii husaidia kuipa huduma ya kanisa lao sura, lakini kwa wengine inaweza kuwa kama mtihani bila ufatiliaji. Wakati nilipokuwa sehemu ya mpango huu, nikiwa askari na afisa wa kikao, niligundua kwamba watu waliokuwa na hamu ya kufanya mtihani huu walikuwa wa umri angalau wa miaka 30. Wale walio wadogo waliulizwa, lakini mara nyingi hawakuhimizwa waliposahau au hawakuhangaishwa (ikitegemea ni nani alikuwa anazungumza juu ya vijana hawa) kujibu maswali ya kuhojiana. Kwa hiyo 'maono' yetu kwa mwaka ujao yalitegemea zaidi mchango kutoka kwa watu ambao hawakuwakilisha kanisa letu lote katika jamii.

Kama nimeaibika, nikitafakari kuhusu haya miaka kadhaa iliyopita, ninaamini tunaweza kutumia juu ya haya miaka kadhaa baadaye, naamini tunaweza kutumia kifungu hiki cha Biblia kwenye mada ya 'Utofauti wa Vizazi'. Mwili wa Kristo sio tu jumla ya mkusanyiko wa karama, lakini ni jumla ya watu wote walio na karama.

Kulifanya hili liwe wazi kidogo, ningependa kutumia maneno ya 'huduma ya vizazi vingi' na 'huduma kati ya vizazi'. Adcock[1] anaeleza kwamba huduma ya vizazi vingi huonekana wakati vizazi vyote viko pamoja katika chumba kimoja lakini hawaingiliani wala hawachangamani. Fikiria kuhusu kikao ambacho wakati wa ibada watoto wanakwenda kwenye kusanyiko lao. Au, baada ya ibada kahawa na chai huwepo na watu wanaonekana kushirikiana vizuri, lakini ukitizama kutoka mbali kidogo, unagundua kwamba watu wazima wanazungumza wao kwa wao, wazazi pamoja na wale ambao nao wana watoto, wana muziki na wana muziki na vijana hukaa mahali fulani kwenye kona wakishughulika na ya kwao, n.k. Sasa, huduma kati ya vizazi huhimiza vizazi vichangamane; watu wasikae na wale ambao wanajisikia vizuri kukaa nao – kundi lao wenyewe na/au kizazi, lakini 'wavuke chumba' kuzungumza na wengine.

## 'TUNATAKIWA KUWA WENYE KUJALI KARAMA ZINAZOTOLEWA NA ROHO KWA KILA MMOJA.'

Katika Biblia, tunaweza kupata mifano mingi ya mahusiano kati ya vizazi tofauti:

- Paulo aliyemwelekeza Timotheo asimruhusu yeyote amdharau kwa sababu ya ujana wake lakini alimhimiza aongoze jamii yake (1 Timotheo 4)


- Eli aliyemshauri Samweli baadaye alihitaji maelezo juu ya nani aliyekuwa akimwita usiku wa manane. Baadaye, Samweli alikuja akawa mshauri wa Daudi ambaye – kwa kuwa alikuwa mtoto mdogo – hakutarajiwa na baba yake mwenyewe kuwa anastahili.

- Naomi aliyemwelekeza na kumshauri Ruthu katika njia za Waisraeli. Ruthu, mgeni kutoka Moabu, alikuja kuwa bibi mkubwa wa Daudi.

Badala ya kutazama uwezekano unaoweza kuletwa na vizazi tofauti, huwa tuna tabia ya kuangalia mambo yanayotishia yale ambayo kizazi chetu wenyewe kinayachukua kuwa ya muhimu. Kwa mfano: vizazi vikongwe hutumia miaka mingi wakijenga 'hali yao' na kujisikia wanatishiwa na 'wale wanaowafuata'. Vizazi vichanga vinaweza kuona mwenendo huu kuwa ni kikwazo cha maendeleo na ubunifu.[2]

---

1 Adcock, G. (2020) The Essential Guide to Family Ministry (p. 105-p. 118)
2 Satterwhite, A.L. (28 May 2020) https://outcomesmagazine.com/embracing-generational-diversity/



## JADILI:

* Unatambua namna gani kikao chako kwenye uwigo kati ya vizazi vingi na kati ya vizazi?
* Tazama mahali palipotajwa pa kuanzia: unafikiri Mungu anakuambia ukabiliane na lipi kwanza? Unafikiri utatakiwa kuzungumza na nani ili uanzishe utaratibu huu?

Kupita katika Biblia yote tunaona kwamba Mungu huviita vizazi kwake na kwa kila mmoja. Hatutakiwi kufuata mfano huo kwa kuwajali wengine na kuthamini kile ambacho kila mmoja anaweza kutoa kwenye jamii ya kanisa? Mara ya mwisho ilikuwa lini ulipomwendea mtu ambaye hakuwa wa kizazi chako na ukamsikiliza kwa makini – bila ya kuwa na ajenda – upate kumfahamu tu? Mara ya mwisho kwako kumwalika mtu ajifunze kutoka kwako ilikuwa lini?

Tuanzie wapi? Adcock[1] anatoa sehemu kadhaa za kufikiria kuanzia katika hamu ya kutaka kuuonyesha kwa kweli 'mwili wa Kristo, mahali ambapo kila mmoja wenu ni sehemu yake' (1 Wakorintho 12:27).

### MAHALI PA KUANZIA:

**1. Mkusanyiko:** lini na wapi huwa na vizazi mbalimbali pamoja katika chumba kimoja? Jaribu kufanya wakati huu uwe wakati wa kuelewa, kuwafikia wengine – kutoa hali ya kuwa mwili mmoja. Fikiria sura ya Agano la Kale ya sherehe: chakula cha ushirika mahali ambapo kila mmoja anakaribishwa kwani anadhihirisha kabila la Mungu.

**2. Kujenga mahusiano**: unganisha! Kwa kuzungumza pamoja unapata uelewa zaidi wa uzee unafananaje au kuwa mdogo kukoje katika siku hizi. Kwako wewe ina maana gani kuwa mwanafunzi wa Kristo?

**3. Kuimarisha ibada:** hii haina maana ya kuongeza ibada nyingine au ibada tofauti ya kuabudu. Ni kuhusu kutengeneza akili katika maisha yote ya kikao na shughuli zake: 'kila mmoja, bila kujali umri, anaweza kufikia na kujisikia yeye ni sehemu ya 'kabila' au jamii, mwenye uwezo wa kupokea msaada inapohitajika na kutumika kwa manufaa ya wengine. Ni kuhusu kila mwana chama, kutoka yule mdogo hadi yule mkubwa, wakitambua kwamba wao ni sehemu ya jamii pamoja na wengine wakiwa na nafasi ya kushiriki kikamilifu.[1]

**4. Uongozi:** Tunahitaji watu kutoka vizazi vyote katika uongozi. Mamlaka yanaweza kuwa wajibu wa pamoja – umri wote wana vingi vya kupokea na kutoa kwa kila mmoja. Waweke watu wako kuzunguka meza. Usiwaalike tu waje mara chache kuja kutoa mawazo yao, lakini wafanye wawe wanatoa maamuzi.

'Mungu hutualika sisi kuwa washirika pamoja naye kama anavyofanya zaidi bila kikomo cha tunayopokea peke yetu. Wewe na mimi hatuna kikomo cha tumaini letu binafsi na ndoto zetu, hata kama zinaweza kuwa za kufurahisha namna gani.' - Marcus Overstreet[3]

3 Overstreet, M. (13 July 2019) https://ourbestdays.org/blog/generational-thinking

Bwana, na utukuzwe katika vizazi vyote. Tusaidie tuweze kuonana na wenzetu kupitia kwenye macho yako ya upendo. Amina.

**KAPTENI WILLEKE VAN DER WOUDE-VAN DE VENIS**
UHOLANZI, JAMHURI YA CZECH NA SLOVAKIA
Kapteni Willeke ametumika kama afisa wa kikao na kama kasisi. Sasa ana ratibu mpango wa kila juma katika kikao na jamii katika kituo Amsterdam-Mashariki. Watoto wake ambao ni watu wazima wako chuo kikuu na bado wanaishi nyumbani. Willeke ana shauku ya watu.





JESHI LA WOKOVU

Imetolewa 2023
Jeshi la Wokovu Makao Makuu ya Kimataifa
101 QUEEN VICTORIA STREET, LONDON EC4V 4EH